
# MASOMO YA BIBLIA KATIKA MATAYO



**“Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.”**
—Matayo 6:33

# DIBAJI

Kitabu hiki kidogo cha somo la Biblia katika Matayo kimeandikwa kwa YE YOTE atakayependezwa na toleo rahisi a hadithi ya Injili ya ajabu! Hakuna ujumbe mkuu wa kuambia ulimwengu kama huu!

Inatumainiwa kwamba wafanyakazi wengi wa kimisheni kote ulimwenguni watasaidiwa na kijitabu hiki kidogo kwa kulielewa vema neno hili la Mungu lililoko katika kijitabu hiki, pia kitawasaidia wengi kumjua Yesu na kuwa Mwokozi wao wa binafsi katika maisha yao; ikiwa hawajaacha dhambi, waache. Dua letu ni kwamba kitabu hiki kimtie moyo kila msomaji ili aishi maisha yanayompendeza Bwana akijiweka wakfu kwa kumpendeza Bwana Yesu Kristo kila siku—yeye aliyetupa uzima wa milele!

1963 na Bi Rose A. Goodman, Mwandishi

**"FURAHA" yaani kicha cha somo hili kutoka katika kitabu cha Matayo limechapishwa kuwa kusudi la imani:**

**na World Missionary Press, Inc.**
**P.0. Box 120**
**New Paris, Indiana 46553 U.S.A.**

www.wmpress.org

Picha ya jalada na Andrew Beverly.

Bible text copyright by United Bible Societies, Africa Regional Centre, Nairobi, Kenya. Used by permission.

# SOMO LA 1. KUZALIWA KWA YESU KRISTO MWOKOZI WETU



(Matayo 1:18-25)

Basi, hivi ndivyo Yesu Kristo alivyozaliwa: Maria, mama yake, alikuwa ameposwa na Yosefu. Lakini kabla hawajakaa pamoja kama mume na mke, alionekana kuwa mja mzito kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Yosefu, mumewe, kwa vile alikuwa mwadilifu, hakutaka kumwaibisha hadharani; alikusudia kumwacha kwa siri. Alipokuwa bado anawaza jambo hilo, malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akamwambia, "Yosefu, mwana wa Daudi, usiogope kumchukua Maria mke wako, maana amekuwa mja mzito kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Atajifungua mtoto wa kiume, nawe utampa jina Yesu, maana yeye atawaokoa watu wake kutoka katika dhambi zao." Basi, haya yote yalitukia ili litimie lile neno Bwana alilosema kwa njia ya nabii: "Bikira atachukua mimba, atamzaa mtoto wa kiume naye ataitwa Emanueli" (maana yake, "Mungu yupo pamoja nasi.") Hivyo, Yosefu alipoamka usingizini alifanya kama huyo malaika alivyomwambia, akamchukua mke wake nyumbani. Lakini hakumjua kamwe kimwili hata Maria alipojifungua mtoto wa kiume. Naye Yosefu akampa jina Yesu.

## JAMBO LA KUFANYA

A. Baada ya kila swali kuna nafasi iliyowazi, itumie nafasi hii kwa kuandika jina lako. Ikiwa huwezi kujibu swali, soma tena maandiko. Majibu yote ya somo hili yanapatikana katika hadithi hii.

1. Mama wa Yesu aliitwa nani?..............................

2. Mariamu mama wa Yesu alikuwa mja mzito kwa uwezo wa ..................................................


Jambo hili linatuonyesha kwamba Mungu ndiye Baba wa Yesu kwa sababu Roho Mtakatifu na Mungu ni Mtu Mmoja.

3. ..............................alimtokea Yosefu kwa ndoto akamwambia kwamba, "Usiogope kumchukua Mariamu mke wako, maana amekuwa mja mzito kwa uwezo wa Roho Mtakatifu."

4. Neno "Emanueli" lina maana............ ............ .................... (maneno matatu)

B. Jifunze kifungu hiki: "Nawe utampa jina YESU, maana yeye atawaokoa watu wake kutoka katika dhambi zao."— Matayo 1:21

## SABABU ZA KUONYESHA YESU NI MWOKOZI WA DHAMBI ZETU




Baba yake Yesu hakuwa mwanadamu. Roho Mtakatifu ndiye Baba Yake. Kwa hivyo damu yake ni takatifu. Hii ndiyo sababu alikufa msalabani kwa dhambi zetu. Yesu alikuwa sadaka takatifu ya ondoleo la dhambi kwa sababu hakuwa na dhambi. Yesu ni mtakatifu. Kusudi la kuja hapa ulimwenguni ni kutuokoa dhambini! Hii ndiyo sababu inayotufanya kumwita Mwokozi wetu. Alikuja kutuokoa.

## YESU NI MUNGU —
## ALIKUJA KATIKA MWILI WA MWANADAMU

# SOMO LA 2. WATAALAM WA NYOTA KUTOKA MASHARIKI WALIMTEMBELEA YESU



(Matayo, Mlango wa Pili)

Yesu alizaliwa mjini Betlehemu, Yudea, wakati Herode alipokuwa mfalme. Punde tu baada ya kuzaliwa kwake, wataalamu wa nyota kutoka mashariki walifika Yerusalemu, wakauliza, "Yuko wapi mtoto, Mfalme wa Wayahudi, aliyezaliwa? Tumeiona nyota yake ilipotokea mashariki, tukaja kumwabudu." Mfalme Herode aliposikia hayo, alifadhaika, yeye pamoja na wakazi wote wa Yerusalemu. Basi, akawaita pamoja makuhani wakuu wote na walimu wa Sheria, akawauliza, "Masiha atazaliwa wapi? Nao wakamjibu, "Mjini Betlehemu, mji wa Yudea. Ndivyo nabii alivyoandika: 'Ewe Betlehemu katika nchi ya Yuda, kwa vyo vyote wewe si mdogo kabisa kati ya viongozi wa Yuda; Maana, kwako atatokea kiongozi atakayewaongoza watu wangu Israeli.' " Hapo, Herode aliwaita faraghani hao wataalamu wa nyota, akawauliza wakati hasa ile nyota ilipowatokea. Kisha akawatuma Betlehemu akisema, "Nendeni mkapeleleze habari za mtoto huyo. Mkisha mpata nileteeni habari ili nami niende nikamwabudu." Baada ya kumsikiliza mfalme, hao watalaamu wa nyota wakaenda. Kumbe ile



nyota waliyokuwa wameiona upande wa mashariki iliwatangulia hata ikaenda kusimama juu ya mahali pale alipokuwa mtoto. Walipoiona hiyo nyota, walifurahi mno. Basi, wakaingia nyumbani, wakamwona yule mtoto pamoja na Maria mama yake; wakapiga magoti, wakamsujudia. Kisha wakafungua hazina zao, wakampa zawadi: dhahabu, ubani na manemane. Mungu aliwaonya katika ndoto wasimrudie Herode; hivyo wakarudi makwao kwa njia nyingine. Baada ya wale wageni kuondoka, malaika wa Bwana alimtokea Yosefu katika ndoto, akamwambia, "Amka! Mchukue mtoto pamoja na mama yake, mkimbilie Misri. Kaeni huko mpaka nitakapokuambia, maana Herode anakusudia kumwua huyu mtoto." Hivyo, Yosefu akaamka, akamchukua mtoto pamoja na mama yake akaondoka usiku, akaenda Misri. Akakaa huko mpaka Herode alipokufa. Jambo hilo lilifanyika ili neno alilosema Bwana kwa njia ya nabii litimie: "Nilimwita Mwanangu kutoka Misri." Herode alipogundua kwamba wale wataalamu wa nyota walikuwa wamemhadaa, alikasirika sana. Akaamuru watoto wote wa kiume katika Betlehemu na kando kando yake wenye umri wa miaka miwili na waliopungua umri huo wauawe. Alifanya hivyo kufuatana na muda aliopata kujua kutoka kwa wale wataalamu wa nyota. Ndivyo yalivyotimia maneno yaliyosemwa kwa njia ya nabii Yeremia: "Sauti imesikika mjini Rama, kilio na maombolezo mengi. Rakeli anawalilia watoto wake, wala hataki kutulizwa, maana wote wamefariki." Baada ya kifo cha Herode, malaika wa Bwana alimtokea Yosefu katika ndoto kule Misri, akamwambia, "Amka! Mchukue mtoto pamoja na mama yake, urudi tena katika nchi ya Israeli, maana wale waliotaka kum-



**wua mtoto huyo wamekwisha kufa." Basi, Yosefu aliamka, akamchukua mtoto pamoja na mama yake, akarejea katika nchi ya Israeli.**

**Lakini Yosefu aliposikia kwamba Arkelao alikuwa mfalme wa Yudea mahali pa baba yake, aliogopa kwenda huko. Baada ya kuonywa katika ndoto, alikwenda katika mkoa wa Galilaya, akahamia katika mji uitwao Nazareti. Ndivyo yalivyotimia maneno yaliyonenwa kwa njia ya manabii: "Ataitwa Mnazare."**

## JAMBO LA KUFANYA

A. Maswali yaliyoko hapa chini yaweza kujibiwa kwa neno NDIYO au LA. Ikiwa jibu ni ndiyo, andika kwa herufi kubwa NDIYO katika nafasi iliyoachwa wazi. Na jibu likiwa la, andika kwa herufi kubwa LA katika nafasi iliyoachwa wazi baada ya swali.

1. Je, Yesu alizaliwa Bethlehemu ya Yudea?.........
2. Wataalam wa nyota waliona nyota mashariki?..
3. Je, mfalme Herode alifurahi kusikia kwamba Yesu amezaliwa?...............
4. Je, wataalam wa nyota walirudi kumweleza Herode mahali mtoto Yesu alipokuwa?............
5. Je, malaika wa Mungu alimwambia Yosefu kukimbilia Misri? ................
6. Je, mfalme Herode aliwaua watoto wote wadogo waliokuwa na miaka miwili kwenda chini waliokuwa Bethlehemu na kando yake? ............

B. Jaza nafasi zilizowazi na maneno yanayokosekana kutoka kwa hadithi hii uliyoisoma.

"Na walipoingia nyumbani wakamwona yule mtoto pamoja na .................... mama yake, wakapiga magoti, wakamsujudia, kisha wakafungua hazina zao, wakampa ........................; ...................., ubani, na ..............................

## SADAKA YA KWANZA

Sadaka ya kwanza aliyoletewa Yesu ililetwa na wataalam wanyota kutoka mashariki. Zawadi ya dhahabu ilikuwa ni alama ya fahari ya ufalme. Ubani na manemane ulikuwa ni ulimbo wa manukato uliotolewa kwa miti iotayo upande wa mashariki, dhahabu ni vitu vya dhamani kwa mwanadamu. Manemane ilimaanisha utu, yaani kuzaliwa katika mwili wa mwanadamu na mazishi yake. Manemane ilimaanisha kielelezo cha Umungu wake. Huenda tusimpe Yesu zawadi za maana kama hizi, lakini twaweza kujitoa kwake kuwa zawadi kuu.

## WATAALAM WA NYOTA WALIMSHUJUDU YESU

Tunaona kwamba katika hadithi ya pili wataalam wa nyota walimwabudu Yesu! Hawakumwabudu Maria. Maria alikuwa mama wa Yesu wa hapa ulimwenguni. Naye Yesu alipokufa alimkabithi mamaye kwa Yohane. Katika mlango wa 19 wa Yohane, mstari wa 26 na 27, tunasoma, "Yesu alipomwona mama yake, na karibu naye amesimama yule mwanafunzi aliyempenda, akamwambia mama yake: Mama! Tazama, huyo ndiye mwanao! Halafu akamwambia yule mwanafunzi: Tazama, huyo ndiye mama yako!" Hapa twaona kwamba Yesu hakumwita mama, lakini alisema, mwanamke! Ni lázima tuwe waangalifu na tumwabudu Bwana Yesu Kristo pekee; aliye Mwokozi wetu. Tusiabudu sanamu yo yote au binadamu mwingine! Kumbuka katika hadithi ya kwanza tulisoma kwamba jina lingine la Yesu ni EMANUELI maana yake ni Mungu pamoja nasi! Hii inatufundisha kwamba Yesu pia ni Mungu! Yesu alipokuja

ulimwenguni ilikuwa ni siku ya ajabu; alikuwa mtoto mdogo, akakua kati ya wanaume na wanawake. Yeye ni Mungu aliyeonekana na watu katika hali ya mwili. (Soma Yohana 1:1, 14 na Wakolosai 2:9 na Matayo 12:50).

## SOMO LA 3. YESU ABATIZWA NA YOHANE MBATIZAJI



(Matayo 3:1-6 na 13-17)

**Siku hizo Yohana Mbatizaji alitokea, akaanza kuhubiri katika jangwa la Yudea: "Tubuni, maana utawala wa mbinguni umekaribia." Huyu Yohana ndiye yule ambaye nabii Isaya alinena juu yake aliposema: "Sauti ya mtu imesikika jangwani: 'Mtayarishieni Bwana njia yake, nyosheni vijia vyake.' " Yohana alivaa vazi lililoshonwa kwa manyoya ya ngamia, na ukanda wa ngozi kiunoni mwake. Chakula chake kilikuwa nzige na asali ya mwituni. Basi, watu kutoka Yerusalemu, kutoka mkoa wote wa Yudea na sehemu zote za kando kando ya mto Yordani, walimwendea, wakaziungama dhambi zao, naye akawabatiza katika mto Yordani. Wakati huo Yesu alitoka Galilaya akafika katika mto Yordani, akamwendea Yohana ili abatizwe naye. Lakini Yohane alijaribu kumzuia akisema, "Je, wewe unakuja kwangu? Mimi hasa ndiye ninayehitaji kubatizwa nawe." Lakini Yesu akamjibu, "Acha tu iwe hivyo kwa sasa, maana kwa namna hii inafaa tuyatekeleze yale yote Mungu anayotaka." Hapo Yohana akakubali. Mara tu Yesu alipokwisha batizwa alitoka majini, na ghafula mbingu zilifunguka, akaona Roho wa Mungu akishuka kama njiwa na kukaa juu yake. Sauti kutoka mbinguni ikasema "Huyu ndiye Mwanangu mpenzi, nimependezwa naye."**

## JAMBO LA KUFANYA

Jaza nafasi zilizowazi na maneno yaliyosawa. Majibu yote yanapatikana katika hadithi ya tatu.

1. Yohana Mbatizaji alihubiri ujumbe huu: "Tubuni, maana utawala wa .................... umekaribia."
2. Yohana alikula .................. na ....................
3. Nani aliyemjia Yohane akitaka kubatizwa?......
4. Mara tu Yesu alipotoka majini, Roho wa Mungu akashuka kwake kama ..............................
5. Sauti kutoka mbinguni ikasema: "Huyu ndiye .................... mpenzi nimependezwa naye."

## NINI MAANA YA KUTUBU?

Kutubu inamaana kusikitikia kosa ulilolifanya huku ukiwa na nia kwamba ungefanya wema tu; unasikitika na kutamani kwamba ungefanya wema kila siku. Kutubu inamaana kugeuka au kuacha kutenda mabaya na kutenda mema. Mambo mabaya tunayoyafanya yanaitwa dhambi. Kitu cho chote kisichompendeza Mungu ni dhambi. Isipokuwa toba la kweli mara hutuletea badiliko mioyoni mwetu. Siku moja msichana mdogo alisema: "Kutubu ni kusikitika kabisa na kuondoka kabisa." Tukiomba kwa Yesu, atatusaidia kutupa nguvu na kutuondoa kabisa kwenye maovu. Yesu anauwezo wa kubadili mioyo yetu ya dhambi na kuwa mioyo misafi. Atatuondolea mbali dhambi zetu na kutujaza na Roho wake. Je, umemwuliza Yesu kila siku kukupa nguvu za kutenda mambo yanayompendeza?

Msichana huyu mdogo anamwomba Yesu. Anatubu, anamwambia Yesu kwamba amesikitika kwa




dhambi zake. Anasikitika kwa mabaya yote aliyofanya. Yesu atasikia maombi yake na kumsamehe. Atamsaidia kufanya yaliyomema tu. Atampa moyo msafi. Kwa msichana huyu kumwomba Yesu kila siku kumfanya kuwa mwenye nguvu za kufanya mambo yatakayompendeza Yesu.

USHUHUDA WA PEKEE

Utukufu wa Mungu ulikuwa katika ubatizo maalum wa Yesu Kristo. (1) Mungu Baba, aliyezungumza kutoka mbinguni, akisema, "Huyu ndiye mwanangu mpenzi, nimependezwa naye." (2) Mungu mwana, aliyebatizwa na Yohana Mbatizaji. Jina lake la kibinadamu aliitwa Yesu kwa sababu alikuja kutuokoa kutoka dhambini. (3) Mungu yaani Roho Mtakatifu, alishuka chini kutoka mbinguni kama njiwa akakaa juu yake. Ni ajabu kwa upendo wa Mungu kutujia sisi kwa njia hizi tatu!

## SOMO LA 4. YESU AJARIBIWA NA IBILISI

(Matayo 4:1-11)

**Kisha Roho alimwongoza Yesu mpaka jangwani ili ajaribiwe na Shetani. Akafunga**



siku arobaini kutwa kucha, na mwishowe akaona njaa. Basi, mshawishi akamjia, akamwambia, "Ikiwa wewe ni Mwana wa Mungu, amuru mawe haya yawe mikate." Yesu akajibu, "Imeandikwa katika Maandiko matakatifu: 'Binadamu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno asemalo Mungu.' " Kisha Shetani akamchukua mpaka Yerusalemu, mji mtakatifu, akamweka juu ya mnara wa Hekalu, akamwambia, "Ikiwa wewe ni Mwana wa Mungu, jitupe chini; maana imeandikwa: 'Mungu atawaamuru malaika wake kwa ajili yako; watakuchukua mikononi mwao usije ukajikwaa kwenye jiwe.' " Yesu akamwambia, "Imeandikwa pia: 'Usimjaribu Bwana, Mungu wako.' " Kisha Shetani akamchukua mpaka juu ya mlima mrefu, akamwonyesha tawala zote za ulimwengu na fahari zake. akamwambia, "Hivi vyote nitakupa kama tu ukipiga magoti na kuniabudu." Hapo, Yesu akamwambia, "Nenda zako Shetani! Imeandikwa: 'Utamwabudu Bwana Mungu wako na kumtumikia yeye peke yake.' " Basi, Shetani akamwacha, na malaika wakaja, wakamtumikia.

## JAMBO LA KUFANYA

A. Jibu maswali yaliyoko hapa chini, majibu yanapatikana katika hadithi ya nne.

1. Kufunga inamaana kushinda bila kula chakula. Yesu alishinda siku ngapi bila kula chakula?............
2. Ni nani aliyekuja kumjaribu Yesu jangwani?....
3. Shetani alitaka Yesu kujitupa chini kutoka juu ya mnara wa ...............................
4. Shetani alitaka Yesu kugeuza mawe kuwa.......
5. Shetani alitaka Yesu ampigie magoti na ...........

B. Jifunze kifungu hiki cha kukumbuka: "Utamwabudu Bwana Mungu wako na kumtumikia yeye peke yake." — Matayo 4:10

## YESU HAMTII IBILISI

Ibilisi alijaribu kumwamrisha Yesu kumtii. Yesu alifahamu sauti ya Shetani. (Jina lingine la Shetani ni Ibilisi, jina ambalo limetumika katika hadithi hii ya nne.) Ibilisi alitaka kumjaribu Yesu ili atumie uwezo wake kwa njia mbaya. Hili linaitwa jaribu. Alijaribu kumjaribu Yesu kufanya ubaya. Lakini Yesu hakumtii Ibilisi hata kidogo. Kwa hiyo Yesu alimshinda Ibilisi na hakufanya dhambi. Majaribu matatu yalimjia Yesu lakini Yesu hakulitii jaribu lo lote! Kumbuka kwamba Ibilisi alitaka Yesu kumpigia magoti na kumwabudu! Kwa hivyo nasi tusimwabudu Ibilisi! Ni vibaya sana. Yesu angekuwa na haja ya utajiri wa vitu vya ulimwengu huu angemsikiliza Shetani na kumtumikia. Ni lazima tuwe waangalifu pia. Tusijaribu kupata utajiri wa aibu kwa kutenda uovu kama kusema uwongo au kuiba au kumkana Bwana wetu Yesu Kristo. Ni lazima tumweke Yesu mbele katika maisha yetu na kufanya mapenzi yake hata ingawa tutakuwa maskini. Yesu alijiweka katika hali ya umaskini ili tupate uzima wa milele ili kwamba siku moja twende kukaa naye milele. (2 Wakorinto 8:9)

Tusitumie uwezo wetu kwa njia mbaya hata kidogo. Tujaribu kila siku kutii sheria za kimwili na kutunza miili yetu. Yesu alitufundisha alipokataa kujitupa chini kutoka kwa kinara kirefu cha sinagoji. Tunajifunza kwamba, tusidhuru miili yetu kwa kusudi la kujitakia makuu ya aibu.

## SIRI AMBAYO YESU ALIITUMIA


Mara kwa mara Ibilisi alimjaribu Yesu ili afanye

maovu, Yesu alitumia NENO LA MUNGU. Hili ndilo jambo unalostahili kufanya. Mungu ametupa Biblia tuisome. Biblia ni Neno la Mungu. Kwa kuisoma Biblia tunakuwa na nguvu. Ni muhimu tukariri vifungu vya Biblia ili vitusaidie kumshinda Ibilisi. Jaribu linapotufikia — siyo kwamba tumetenda dhambi; bali kulitii jaribu, ndipo kutenda dhambi. Katika Waebrania 4:15 twasoma kwamba Yesu "alijaribiwa kama sisi kwa kila namna lakini hakutenda dhambi." Yesu hakutii majaribu ya Ibilisi!

KUMBUKA HAYA

Sauti inayokujia kukujaribu ufanye mabaya ni sauti ya Shetani. Si sauti ya Mungu! Mara moja mwombe Yesu akupe nguvu ili usiitii sauti ya Shetani. Shetani anapoona kwamba hawezi kukujaribu ufanye maovu, atatoka kwako na kukuacha jinsi Ibilisi alivyomwacha Yesu.

## SOMO LA 5. YESU AWACHAGUA WASAIDIZI



(Matayo 4:17-22)

**Tangu wakati huo Yesu alianza kuhubiri na kusema, "Tubuni, maana Utawala wa mbinguni umekaribia!" Yesu alipokuwa anatembea kando ya ziwa Galilaya aliwaona ndugu wawili wavuvi: Simoni (aitwaye Petro) na Andrea, ndugu yake, wakivua samaki ziwani kwa nyavu. Basi, akawaambia, "Nifuateni nami nitawafanya ninyi wavuvi wa watu." Mara wakaziacha nyavu zao, wakamfuata. Alipokwenda mbele kidogo, aliwaona ndugu wengine wawili: Yakobo na Yohana, wana wa Zebedayo. Hao walikuwa ndani ya mashua pamoja na baba yao Zebedayo wakizitengeneza nyavu zao. Basi, Yesu akawaita, nao mara wakaiacha mashua pamoja na baba yao, wakamfuata.**

## JAMBO LA KUFANYA

A. Jibu maswali yafuatayo ukijaza katika nafasi zilizo wazi. Majibu yote yanapatikana katika hadithi ya tano.

1. Ndugu ya Simoni Petro aliitwaje? ......................
2. Ndugu hawa wawili walikuwa wakitupa nini baharini? ...................................
3. Yakobo mwana wa Zebedayo naye alikuwa na ndugu. Ndugu yake aliitwaje? .........................

## MWITO MKUU WA KUMFUATA YESU

Huenda wavuvi hawa wawili walikuwa na furaha sana kuitikia mwito wa Bwana Yesu alipowaamuru wamfuate! Mara tu walitii na wakamfuata kwa furaha. Badala ya kuvua samaki kwa kutumia nyavu zao watakuwa wavuvi wa kuvuta watu kwa Yesu. Yesu anahitaji wafuasi wengi. Ni kweli kwamba anahitaji sisi sote kumfuata! Je, unamfuata Yesu? Ikiwa hufanyi hivyo, je, una sababu inayokufanya usimfuate? Je, umefikiri kuhusu jambo hili? Mwito mkuu ambao tungeuitikia ni mwito wa Yesu. Tumfuate yeye; kwa kumfuata kuna maana ya kuupata uzima wa milele. Katika kitabu cha Yohana mlango wa 14, mstari wa 6, Yesu anasema, "Mimi ni njia, ukweli na uzima: hakuna awezaye kwenda kwa Baba ila kwa kupitia kwangu."

## SOMO LA 6. YALE YESU ALIYOYAFUNDISHA

(Matayo 5:1-12)

**Yesu alipoyaona makundi ya watu alipanda mlimani, akaketi. Wanafunzi wake wakamwendea, naye akaanza kuwafundisha: "Heri wanaojiona kuwa maskini mbele ya Mungu, maana Utawala wa**

**mbinguni ni wao. Heri walio na huzuni, maana watafarijiwa. Heri wapole, maana watapewa nchi. Heri walio na njaa na kiu ya kufanya atakavyo Mungu, maana watashibishwa. Heri wenye huruma, maana watahurumiwa. Heri wenye moyo safi, maana watamwona Mungu. Heri wenye kushughulikia amani, maana wataitwa watoto wa Mungu. Heri wanaoteswa kwa sababu ya kufanya atakavyo Mungu, maana Utawala wa mbinguni ni wao! Heri yenu ninyi kama watu wakiwatukana, wakiwadhulumu na kuwasingizia kila aina ya uovu kwa sababu yangu. Furahini na kushangilia maana tuzo lenu ni kubwa mbinguni. Hivyo ndivyo watu walivyowadhulumu manabii waliokuwako kabla yenu."**

## HERI WENYE HURUMA

Siku moja mtu mmoja alikuwa akisafiri kupitia kwenye nchi ya hatari alipokutana na mbwa aliyekuwa amejeruhiwa mguu. Mtu huyo alisimama kuuangalia mguu wa yule mbwa, punde si punde akagundua kwamba kulikuwa na mwiba katika mguu wa mbwa huyo. Aliutoa ule mwiba kwa uangalifu, akausafisha mguu wa mbwa yule na akaufunga na kitambaa chake cha kufutia kamasi. Mbwa yule alienda zake.

Baadaye, ilikuwa kwamba mtu huyu alishikwa na maadui. Alikuwa mateka, alitaka kuuawa. Mara tu yule mbwa aliyekuwa ndiye mashuhuri kwa mbwa wote wa yule adui alimkimbilia yule mfungwa na akaanza kumlamba mikono yake na kumwonyesha furaha na upendo wa kila namna. Baadaye yule mkuu wa maadui akagundua kwamba mbwa wake aliokolewa na mateka yule. Badala ya kumwua, alimshukuru sana yule mateka wake kwa utabibu wa mbwa wake na akamwacha huru. "Heri wenye huruma maana watahurumiwa."

## SIFA ZA HERI

Katika hadithi ya sita kuna "heri" tisa. Tunaziita sifa za heri. Hata ingawa Mungu ametupa amri kumi, Yesu alitupa heri tisa tu. Hata hivyo katika Ufunuo mlango wa 22, mstari wa 14, tunapewa heri nyingine: —"Heri yao wale wanaoosha mavazi yao, kwani watakuwa na haki ya kula tunda la mti wa uzima, na haki ya kuingia mjini kwa kupitia milango yake."

## SOMO LA 7. YESU ATUFUNDISHA KUOMBA

(Matayo 6:5-15)

**"Jihadharini msije mkafanya matendo yenu mema mbele ya watu kusudi mwonekane nao. La sivyo, Baba yenu aliye mbinguni hatawapeni tuzo. Basi, unapomsaidia maskini usijitangaze. Usifanye kama wanafiki wafanyavyo katika masunagogi na njiani ili watu wawasifu. Kweli nawaambieni, wamekwisha pata tuzo lao. Lakini wewe unapomsaidia maskini, fanya hivyo kwamba hata rafiki yako asijue ufanyalo. Toa msaada wako kwa siri, na Baba yako aonaye mambo yaliyofichika atakutuza."**

**"Mnaposali, msifanye kama wanafiki. Wao hupenda kusimama na kusali katika masunagogi, na katika pembe za njia ili watu wawaone. Kweli nawaambieni, hao wamekwisha pata tuzo lao. Lakini wewe unaposali, ingia chumbani mwako, na ukisha funga mlango, sali kwa Baba yako asiyeonekana. Naye Baba yako aonaye yaliyofichika atakutuza. Mnaposali, msipayuke maneno kama watu wasiomjua Mungu. Wao hudhani kwamba Mungu atawasikiliza ati kwa sababu ya maneno mengi. Msiwe kama wao. Baba yenu anajua mnayoyahitaji hata kabla ya kumwomba. Basi, hivi ndivyo mnavyopaswa kusali: 'Baba yetu uliye mbinguni: Jina lako litukuzwe, Utawala wako ufike, Utakalo lifanyike duniani kama mbinguni. Utupe leo chakula chetu tunachohitaji; Utuasamehe makosa yetu kama nasi tunavyowasamehe waliotukosea; Usitutie katika majaribu, lakini utuokoe na yule Mwovu.' Maana mkiwasamehe watu makosa yao, Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi pia. Lakini msipowasamehe watu makosa yao, naye Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu."**

## JAMBO LA KUFANYA

A. Baba yetu uliye .................., jina lako litukuzwe, utawala wako ufike. Utakalo lifanyike. ...................... kama ................. Utupe leo ................ chetu tunachohitaji. Utusamehe makosa yetu kama nasi tunavyowasamehe ...................... Usitutie katika majaribu, lakini utuokoe na yule .....................

B. Jifunze sala hii. Ni mfano wa sala na pia ni mwongozo wa maombi yote yaliyo na ukweli.

1. Baba yetu uliye huko MBINGUNI na Mungu ni Baba yetu. Alituumba naye hutupenda.
2. Jina lake lisitajwe kijuujuu tu. Ni lazima liheshimiwe kwa kuwa ni takatifu. Jina lake LITUKUZWE.
3. Mapenzi ya Mungu yanatimizwa mbinguni na ye yote aliyeko huko. Na ni lazima tuombe kwamba mapenzi yake yafanyike hapa chini pia. Ikiwa kila mmoja wetu atafanya namna ya mapenzi yake yalivyo, tutakuwa na ulimwengu uliojaa hitilafu ya namna gani!
4. Tunaweza kumtajia Baba yetu matakwa yetu yote, hata tumwombe kwa chakula chetu cha kila siku. Hutaka kutupa mahitaji yetu yote.
5. Je, tunawasameheje wengine? Yesu atatusamehe jinsi tunavyowasamehe wengine. Hatuwezi kusamehewa na Mungu tukiwa watu wa hasira, ukali, chuki, wivu au ikiwa mioyo yetu imejazwa na ulipizaji wa kisasi. Tunaweza tu kusamehewa na Mungu tukiwa watu wa kusamehe uovu ambao wenzetu hututendea.
6. Mungu anauwezo wote wa kutuokoa sisi kutoka katika makosa na uovu.



(Matayo 6:25-34)

“Ndiyo maana nawaambieni, msiwe na wasiwasi juu ya chakula na kinywaji mnavyohitaji kwa kuishi, wala juu ya mavazi mnayohitaji kwa miili yenu. Je, maisha ni chakula tu au zaidi? Na mwili, je, si zaidi ya mavazi? Waangalieni ndege wa mwituni: hawapandi, hawavuni, wala hawana ghala yo yote. Hata hivyo, Baba yenu wa mbinguni huwalisha. Je, ninyi si bora zaidi kuliko hao? Ni nani miongoni mwenu kwa kuwa na wasiwasi sana anaweza kuuongeza muda wa maisha yake hata kwa siku moja? Na, kuhusu mavazi, ya nini kuwa na wasiwasi? Tazameni maua ya porini jinsi yanavyomea. Hayafanyi kazi wala hayasokoti. Lakini, nawaambieni, hata Solomoni mwenyewe na fahari zake zote hakupata kuvikwa vizuri kama ua mojawapo. Ikiwa, basi, Mungu hulivika hivyo jani la shambani ambalo leo liko na kesho latupwa motoni, je, hatafanya zaidi kwenu ninyi? Enyi watu mlio na imani haba! Basi, msiwe na wasiwasi: ‘Tutakula nini, tutavaa nini!’ Maana hayo yote yanahangaikiwa na watu wasiomjua Mungu. Baba yenu mbinguni anajua kwamba mnahitaji vitu hivyo vyote. Kwa hiyo, zingatieni kwanza Utawala wa Mungu na matakwa yake, na hayo mengine yote mtapewa kwa ziada. Basi, msiwe na hayo mengine yote mtapewa kwa ziada. Basi, msiwe na wasiwasi juu ya kesho; kesho inayo yake. Matatizo ya siku moja yanawatosheni kwa siku hiyo.”

## JAMBO LA KUFANYA

Jifunze kifungu hiki cha kukumbuka: “Kwa hiyo, zingatieni kwanza Utawala wa Mungu na matakwa yake, na hayo mengine yote mtapewa kwa ziada.”

## NDEGE WA ANGANI WANATUFUNZA NINI?

Je, umewahi kuwaona ndege wakiruka angani? Wana furaha. Hawana wasiwasi. Hawana hofu. Huamka kila asubuhi wakiimba. Wanashukuru kila siku kwa chakula wanachopata na kula. Hawana shaka kwa chakula cha kesho. Wanajua kwamba watapata chakula kesho. Wanaamini Mungu atawatunza.

Ni heri wewe nami tuwe kama ndege. Tuwe na furaha tukiimba nyimbo za sifa kwa Mungu kila asubuhi na kila siku. Tusihofu kuhusu chakula chetu cha kesho. Mungu aliyeumba ndege na huwapa chakula cha kila siku atatupa chakula cha kila siku pia. Sisi ni wadhamani kuu kuliko ndege wengi.

## MAUA YANATUFUNZA NINI?

Je, umeyaona maua? Yanapendeza; maua huota mashambani. Yana rangi za kila aina. Mengine huwa meupe sana. Siku moja Yesu alisema kwamba maua haya yamevaa vizuri hata kushinda mfalme Sulemani aliyekuwa tajiri sana! Nayo maua hayana wasiwasi kuhusu mavazi yao, wala hayasemi tutavaa nini? Mungu ameyapa uzuri na huyavalisha na rangi nzuri. Inafaa tujifunze kwa mifano hii na pia tujue kwamba Mungu atatupa mahitaji yetu. Alituumba na anataka tuamini kwamba atatupa vyote.

## JAMBO LA MAANA SANA

Kwanza ni lázima tumtafute Mungu kwanza. Tuwe wa kwanza kumfikiria, tukianzia mioyoni mwetu; tukimweka wa kwanza katika maisha yetu. Ni lazima tumwishie na tumpende kupita vitu vyote vya ulimwengu huu. Tukimweka Yeye kuwa wa kwanza, atatutunza vizuri zaidi kuliko jinsi tunavyojitunza wenyewe!

# SOMO LA 9. WEMA WA MUNGU KWETU



(Matayo 7:7-12)

**"Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtapata; pigeni hodi, nanyi mtakaribishwa. Aombaye hupewa, atafutaye hupata, na apigaye hodi hukaribishwa. Je, kuna ye yote miongoni mwenu ambaye mtoto wake akimwomba mkate atampa jiwe? Au, je, akimwomba samaki atampa nyoka? Kama, basi, ninyi, ingawaje ni waovu, mwajua kuwapa watoto wenu vitu vizuri, hakika Baba yenu wa mbinguni atafanya zaidi: atawapa mema yote wale wanaomwomba. Watendeeni wengine yale mnayotaka wao wawatendee ninyi. Hii ndiyo maana ya Sheria na mafundisho ya manabii."**

## FUNZO LINALOTOKANA NA MAANDIKO TULIYOYASOMA HAPA JUU

1. Mungu hujibu maombi, tunastahili kumwomba yeye tu.

2. Upendo wa Baba yetu aliye mbinguni ni zaidi ya upendo wa wazazi wetu wa hapa duniani. Kwa hivyo Baba Mungu atatupa vitu vilivyo vyema tunapomwomba kwa imani.

3. Anayemhitaji Mungu kwa nia safi atazidishiwa mema.

4. Mafundisho yote ya dini huwa na ukuweli mmoja — tuwafanyie wengine jinsi unavyopenda wakufanyie. Neno "wengine" linamaana ya watu wote na si kwamba ni mtu mmoja tu, na, si wa kabila au wa nchi yako tu bali ni mtu ye yote.

## JAMBO LA KUFANYA

Jifunze kifungu hiki ni cha maana sana, kinaitwa sharti la dhahabu. "Watendeeni wengine yale mnayotaka wao wawatendee ninyi."—Matayo 7:12

## YALE SHARTI LA DHAHABU LIMEFANYA


Watu wanapolitimiza sharti la dhahabu na kulifuata, jambo la ajabu hufanyika. Haya ni baadhi ya mambo yanayofanyika:

1. Hospitali zimejengwa kwa wagonjwa.
2. Maskini, wazee na watoto wasio na wazazi hujengewa mahali pa kutunziwa.
3. Magereza hurekebishwa na kuwa na hali ya kufaa binadamu.
4. Watu wameachiliwa huru. Hawanunuliwi wala kuuzwa kama watumwa.
5. Wakati mwingine maskini hupewa nguo na chakula.
6. Watu hupendana na husaidiana katika shida mbalimbali.
7. Viongozi huweka sheria zinazofaa kuwalinda walio chini yao.
8. Watu hupewa uhuru wa kuabudu Mungu wanavyotaka.

## SWALI ZURI LA KUJIULIZA NI HILI:

Ikiwa huna hakika katika kufuata sharti hili la dhahabu katika maisha yako, au ikiwa hujui jinsi ya kumtendea mgeni, rafiki au adui, jiulize hivi: "Je, ningekuwa yeye, ningependa nifanyiwe nimi?" Ikiwa moyoni mwako utajibu swali hili kwa haki, ni heri ufanye ulivyofikiria hapo utakuwa umefuata Sharti la Dhahabu.

# SOMO LA 10. WAJENZI WA NAMNA MBILI



(Matayo 7:24-29)

**"Kwa sababu hiyo, kila mtu anayeyasikia maneno yangu na kuyazingatia, atafananishwa na mtu mwenye busara, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba. Mvua ikanyesha, mito ikafurika, pepo kali zikavuma na kuipiga nyumba hiyo. Lakini haikuanguka kwa sababu ilikuwa imejengwa juu ya mwamba. Lakini ye yote anayesikia maneno yangu haya bila kuyazingatia, atafananishwa na mtu mpumbavu aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga. Mvua ikanyesha, mito ikafurika, pepo kali zikavuma na kuipiga nyumba hiyo, nayo ikaanguka, tena kwa kishindo kikubwa." Yesu alipomaliza kusema maneno hayo, umati wa watu ukashangazwa na mafundisho yake. Hakuwa kama walimu wao wa Sheria, bali alifundisha kwa mamlaka.**

## JAMBO LA KUFANYA

Jaza nafasi zilizo wazi na neno lililo sawa kutoka kwa hadithi ya 10.

1. Mtu aliyeyasikia maneno ya Yesu na kuyazingatia anafananishwa na .................... aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba.
2. Mtu aliyeyasikia maneno ya Yesu na hakuyazingatia anafananishwa na .................... aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga.

## MJENZI WA BUSARA

Ikiwa mimi na wewe tunapenda kuwa kama yule mjenzi wa busara, ni lazima tuusikie ujumbe wa Yesu na kutenda asemavyo. Maneno ya Yesu yanapatikana katika Biblia. Mambo mengi ya Yesu

yanapatikana katika kitabu tunachokisoma cha Matayo. Tukijenga mambo yetu juu ya Yesu na kumfuata, tutakuwa salama hata ingawa mawimbi yatatujia au misukosuko ya maisha. Neno "mawimbi ya maisha" linamaana ya mtu kupimwa, katika majaribu, mambo magumu unayokabiliana nayo, au mambo ya huzuni yanayomjia. Yesu Kristo ni kama Mwamba. Yeye ni timamu na hatikisiki au kusogezwa. Tukijenga maisha yetu kwake, atatushika kwa nguvu na hakuna kitu kitakachotututoa kwake hata ingawa tutatingizwa. Unataka kuwa yule mjenzi wa busara? Ikiwa ni hivyo, basi umkubali Yesu kuja moyoni mwako sasa. Mwombe aje moyoni mwako. Yeye akupenda. Ufungue mlango wa moyo wako naye atangia.



## OMBI

Bwana, nisamehe kila dhambi ninayo; nifanye kuwa mkamilifu na msafi, ninaomba ukae ndani yangu leo; uniongoze kwa yote ninayosema na kufanya.

Katika kitabu cha Ufunuo, mlango 3, mstari wa 20, Yesu anasema hivi: "Sikiliza! Mimi nasimama mlangoni na kubisha hodi. Mtu akisikia sauti yangu na kufungua mlango, nitaingia nyumbani kwake na kula chakula pamoja naye, naye atakula pamoja nami."


## MJENZI MPUMBAVU

Watu wengine hawatii Neno la Mungu. Husikiliza na kusahau walilolisikia. Watu hawa wanafananishwa na mtu mpumbavu. Anapopigwa na mawimbi ya maisha, hawezi kustahimili bali huanguka kama jengo lililojengwa juu ya mchanga. Hili ni jambo baya. Yeye hakumkubali Yesu kukaa moyoni mwake naye hakutii maneno ya Yesu.

---

"Msijidanganye wenyewe, kwa kusikiliza tu neno lake, bali litekelezeni kwa vitendo." —Yakobo 1:22

## SOMO LA 11. UPEPO NA BAHARI VYAMTII YESU



(Matayo 8:23-27)

**Yesu alipanda mashuani, na wanafunzi wake wakaenda pamoja naye. Ghafula, dhoruba kali ikatokea ziwani hata mawimbi yakaanza kuifunika mashua. Yesu alikuwa amelala usingizi. Wanafunzi wakamwendea, wakamwamsha wakisema, "Bwana, tuokoe, tunaangamia!" Yesu akawaambia, "Enyi watu wenye imani haba; kwa nini mnaogopa?" Basi, akainuka, akazikemea pepo na mawimbi; kukawa shwari kabisa. Watu wakashangaa, wakasema, "Ni mtu wa namna gani huyu? Hata pepo na mawimbi vinamtii!"**

## WIMBI BAHARINI


Yesu na wanafunzi wake walikuwa katika meli kubwa majini. Yesu alichoka na akalala. Alipokuwa akilala, wimbi kubwa lilitokea, lilikuwa kubwa hata likafunika meli hiyo! Wanafunzi waliogopa, nao wakamwamsha Yesu. Huenda Yesu alishangaa kuona

kwamba wanafunzi wake waliogopa hata alipokuwa nao. Alipoiona imani yao ndogo, aliamka na kutuliza upepo wa bahari, ulitulia na kukawa shwari. Wanafunzi wake wakatambua kwamba Yeye Yesu ni tofauti kuliko mtu ye yote waliyemfahamu. Kweli Mtu huyu alikuwa Mwana wa Mungu! Hata upepo na bahari vyamtii.

### JAMBO LA KUKUMBUKA

Hapo zamani mama mmoja na binti zake walikuwa katika meli kubwa. Meli hiyo ilipatwa na msukosuko fulani na ikaanza kuzama. Baadhi ya watu waliokuwako melini waliogopa, lakini huyu mama na binti zake walimpenda Yesu na walimwamini. Unajua jambo ambalo binti yake mkubwa alilomwambia walipokuwa katika shida hii? Alisema, "Mama, bahari ni ya Yesu kwa kuwa aliitengeneza; kwa hivyo tusiende chini ya meli kwa sababu tuko chini ya ulinzi wake." Kwa furaha na huzuni tulishuhudia kwamba wale walioshuka chini ya meli walikufa kwenye maji ya kina ya bahari. Rafiki yangu, kumbuka mambo haya kwamba "HATUWEZI KUPATA DHARA LO LOTE IKIWA YESU YU PAMOJA NASI."

## SOMO LA 12. NI LÁZIMA TUWAAMBIE WENGINE JUU YA YESU



(Matayo 10:28-33)

**"Msiwaogope wale wauao mwili lakini hawawezi kuiua roho. Afadhali zaidi kumwogopa yule awezaye kuuangamiza mwili pamoja na roho motoni. Mbayuwayu wawili**

huuzwa kwa senti tano. Lakini hata mmoja wao haanguki chini bila kibali cha Baba yenu. Lakini, kwa upande wenu, hata nywele za vichwa vyenu zimehesabiwa zote. Kwa hiyo msiogope; ninyi ni bora kuliko mbayuwayu wengi. Ye yote atakayekiri hadharani kwamba yeye ni wangu, mimi pia nitamkiri mbele ya Baba yangu aliye mbinguni. Lakini ye yote atakayenikana hadharani, nami nitamkana mbele ya Baba yangu aliye mbinguni."

## NI LÁZIMA KUMKIRI KRISTO

Yesu Kristo ametuahidi kwamba tukimkiri hapa duniani mbele ya watu, yeye atatukiri mbinguni mbele ya Mungu. Hili ni jambo la ajabu. Kumkiri inamaana kumtetea katika matendo na kwa yale tusemayo. Je, unawaeleza wengine jinsi alivyokufanyia rohoni hata ukapata wokovu? Hayo ndiyo baadhi ya mambo tunayostahili tufanye tukitaka kumkiri mbele ya watu.

Tukimwonea Yesu aibu kwa kutokumtetea na kutomfanyia kazi anavyohitaji tumfanyie, inamaana kwamba tunamkana Bwana wetu mbele ya watu. Tukifanya hivyo tunaufanya moyo wa Kristo kuhuzunika. Kwa hivyo, ni lazima tumwombe Yesu atusamehe na pia tumwamini ili atusaidie kutenda mema yanayomfurahisha. Tukifanya hivyo hatatukana mbele ya Mungu huko mbinguni.

## HATUSTAHILI KUMWOGOPA MWANADAMU

Watu wengine ni waovu sana. Wanafanya mambo mabaya sana kama kuwaua wengine. Isipokuwa hawa huua mwili peke yake, hawawezi kuua roho. Roho ni sehemu iliyomo ndani mwetu ambayo haifi. Miili yetu inapokufa roho hurudi kwa Mungu aliyeiumba. "Basi, kama vile kila mtu hufa mara moja tu, kisha husimama mbele ya hukumu ya Mungu." (Waebra-

nia 9:27) "Kwa hiyo, kila mmoja wetu atatoa hoja yake mbele ya Mungu." (Waroma 14:12) Tunastahili kumtii Mungu peke yake. Soma Mhubiri 12:13 na 14, "Mche Mungu, nawe uzishike amri zake, maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu. Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya."

Mungu atuambia kwamba tusiogope yale wanadamu watakayotutendea. Wanaweza kututendea maovu ya kila aina kama kutuumiza, wanaweza kutuua bali Mungu anasema kwamba tumwamini tu. Mungu anajua mambo yote! Hata anajua nambari ya nywele tulizonazo kichwani mwetu! Mungu anajua mambo yote! Hata anajua wakati ndege wa angani kama zawaridi anapoanguka chini — arthini. Sisi ni wadhamani kuu kuliko zawaridi. Mungu hatatusahau! Katika kitabu cha Waebrania 13, mstari wa 5, Mungu anasema, "Sitakuacha kamwe wala sitakutupa."

## SOMO LA 13. MFANO WA MPANZI



(Matayo 13:1-9 na 18-23)

**Siku hiyo hiyo, Yesu alitoka katika ile nyumba, akaenda kando ya ziwa, akaketi. Makundi mengi ya watu yalikusanyika hata Yesu akapanda mashua, akaketi. Hao watu walisimama kwenye ukingo wa ziwa, naye Yesu akawaambia mambo mengi kwa mifano. "Sikilizeni! Mpanzi alikwenda kupanda mbegu. Alipokuwa akizipanda, nyingine zilianguka njiani, ndege wakaja wakazidonoa. Nyingine zilianguka kwenye mawe ku-**

sikokuwa na udongo mwingi. Zikaota mara kwa vile kulikuwa na kina kidogo tu cha udongo. Jua lilipotokea zilinyauka na kwa kuwa mizizi yake haikuwa na nguvu, zikakauka. Nyingine zilianguka kwenye miti ya miiba. Hiyo miti ya miiba ikakua, ikazisonga. Lakini nyingine zilianguka kwenye udongo mzuri, zikaota, zikazaa: nyingine punje mia moja, nyingine sitini na nyingine thelathini. Mwenye masikio na asikie."

"Basi, ninyi sikilizeni maana ya mfano huo wa mpanzi. Ye yote asikiaye ujumbe wa Utawala bila kuelewa ni kama zile mbegu zilizoanguka njiani; yule Mwovu huja na kunyakua kile kilichopandwa moyoni mwake mtu huyo. Ile mbegu iliyopandwa kwenye mawe ni mfano wa mtu asikiaye ujumbe huo na mara akaupokea kwa furaha; lakini mtu huyo hana mizizi, huendelea kuuzingatia ujumbe huo kwa kitambo tu na wakati taabu au mateso yanapomjia kwa sababu ya ujumbe huo, huanguka mara. Ile mbegu iliyopandwa kwenye miti ya miiba ni mfano wa mtu asikiaye huo ujumbe lakini wasiwasi wa dunia hii na anasa za mali huusonga ujumbe huo hata hubaki hivi hivi bila matunda. Ile mbegu iliyopandwa kwenye udongo mzuri ni mfano wa mtu ausikiaye ujumbe huo na kuuelewa, naye huzaa matunda; na mbegu moja hutoa punje mia, nyingine sitini na nyingine thelathini."

## NINI MAANA YA KUTUMIA MFANO?

Maana ya mfano ni kutoa mealezo kwa kutumia mambo yanayofahamika na watu ili waelewe ukweli wa mambo ya dini.

## JAMBO LA KUFANYA

A. Hapa chini kuna sentensi ambazo zahitaji kukamilishwa.

1. Mbegu zilizoanguka njiani zilidonwa na ............................

2. Mbegu zilizoanguka kwenye mawe mengi hazikuwa na ................ na jua lilipotokea zili .............., na kwa sababu hazikuwa na mizizi ya nguvu, zili ............................

## MAELEZO YA MFANO HUU

B. Isome tena hadithi hii ili upate maana ya mfano huu; halafu ujaze nafasi zilizowazi na maneno yaliyosahihi. Umejaziwa nafasi ya kwanza.

1. Mfano wa mbegu zilizoanguka kando ya barabara unafanana na mtu anayesikia ............... la ufalme wa Mungu lakini hali ................... Kwa hivyo mwovu huja kwake na kumnyang'anya ukweli uliomo moyoni mwake.

2. Mfano wa mbegu zilizoanguka kwenye sehemu za mawe unafanana na mtu aliyesikia .................. naye hulipokea kwa furaha. Na kwa kuwa hana nafasi ya neno hilo moyoni mwake neno hilo haliwezi kuwa na mizizi, mara taabu na mateso yanapomjia yeye ...............................

3. Mbegu zilizoanguka kwenye miiba ni mfano wa mtu anayesikia neno, naye huwa na wasiwasi wa ..................... kama kazi ya nyumbani, kupika, kushona, biashara au kutafuta anasa zake. Tena utajiri wa ulimwengu huu huwadanganya na kuwaacha bila ..............................

4. Mbegu zilizoanguka kwenye udongo mzuri ni mfano wa mtu asikiaye Neno, naye hulielewa. Hulipokea kwa furaha moyoni mwake naye huendelea kumweka Mungu kwanza katika maisha yake. Yeye haruhusu mahitaji yake ya kila siku kuingia moyoni mwake na kuliondoa Neno; tena moyo wake hautamani utajiri wa aibu. Yeye yu macho kwa kuomba akitubu na kumwamini Mungu kwa kumsaidia kufanya mambo yake. Kwa hivyo huzaa ................, mwingine mia, mwingine sitini na mwingine thelathini.

## SWALI — WEWE NI MSIKILIZAJI WA AINA GANI?

Ikiwa hujawa kama mbegu zilizoanguka kwenye udongo mzuri, mwendee Bwana kwa maombi na umruhusu aingie moyoni na maishani mwako; naye atakusaidia kuzaa matunda mengi.

## SOMO LA 14. MSALABA NA TAJI



(Matayo 16:24-28)

**Kisha Yesu akawaambia wanafunzi wake, "Mtu akitaka kuwa mfuasi wangu ni lazima ajikane mwenyewe, auchukue msalaba wake, anifuate. Maana, mtu anayetaka kuokoa maisha yake atayapoteza; lakini mtu anayeyapoteza maisha yake kwa ajili yangu atayapata. Je, mtu atafaidi nini akiupata ulimwengu wote na hali amepoteza maisha yake? Au, mtu atatoa kitu gani kiwe badala ya maisha yake? Maana, Mwana wa Mtu atakuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika wake, na hapo ndipo atakapomlipa kila mtu kadiri ya matendo yake. Kweli nawaambieni, wako wengine hapa hapa ambao hawatakufa mpaka watakapomwona Mwana wa Mtu akija katika Utawala wake."**

### MSALABA WA KILA MTU

Tukitaka kumfuata Yesu ni lazima tujikane wenyewe na tuchukue msalaba na kumfuata Yeye. Yesu alichukua msalaba kwa ajili yangu na yako. Aliuacha utajiri na utukufu wote mbinguni akaja hapa duniani kutuokoa kutoka kifoni na Jehanum na kaburini! Alivumilia shida nyingi kwa ajili yetu. Waebrania 12, mstari wa 2, unatuambia kwamba Yesu, "kwa ajili

ya furaha iliyokuwa inamngojea yeye alivumilia kifo msalabani, bila kujali juu ya aibu yake na sasa anaketi upande wa kulia wa kiti cha enzi cha Mungu." Yesu alirudi mbinguni ambapo kuna utukufu na furaha. Anataka mimi na wewe kumjia ili tukae pamoja naye. Katika Yohana 14, mstari wa 3, Yesu anatuambia kwamba, "Nikienda na kuwatayarishieni nafasi, nitarudi na kuwachukueni kwangu, ili nanyi muwe pale nilipo mimi."

Nini maana ya kujikana wenyewe? Inamaana kwamba kujinyima jambo fulani ili kuwawezesha wengine wanufaike kwa ajili ya kujinyima kwako. Huenda Yesu anapenda ujinyime kutumia senti zako kumi ili zisaidie kueneza injili kwa watu ambao hawajafikiwa na Biblia au wale ambao hawajamwelewa Yesu vizuri! Huenda tungekuomba ujinyime chakula bora kwa muda ili uokoe roho ya mtu mmoja au mgonjwa mmoja kwa kujitoa kwa senti zako kumi. Huenda tungekuuliza kutonunua kitu unacho hitaji, badala yake ukamsaidie maskini au mwenye njaa. Huenda Yesu angependa uende sehemu fulani kuwaambia watu wa huko, juu ya Yesu. Huenda anakuuliza kutunza mtoto asiye na wazazi kwamba umchukue nyumbani mwako na kumtunza. Kuna njia nyingi tunazoweza kujitolea kwazo na kuwasaidia wengine.

## ROHO YAKO INA DHAMANI KUU KULIKO ULIMWENGU HUU

Hata ingekuwa ufanye kazi na kuwa tajiri wa ulimwengu huu bila kumpenda na kumwamini Yesu kuwa Mwokozi wako, ungekuwa mjinga kweli kweli,

kwa sababu roho yako ingepotea! Hakuna faida utakayoipata ukipoteza uzima wa milele! Je, mtu aweza kuibadili roho yake na nini? Kulikuwa na mtu mmoja ambaye alitaka kuwapendeza jamaa yake kuliko Mungu. Kwa njia kama hii, alibadili roho yake na mambo ya kawaida yanayosemekana kuwa mema hapa ulimwenguni. Hakuna kishawishi cho chote hapa ulimwenguni ambacho chaweza kuwa sawa na roho ya mtu. Tujihadhari tusifanye kitu kitakachotupoteza ili tumwache Bwana Yesu Kristo.

JAMBO LA KUFANYA

Jifunze mstari huu. Matayo 16:27 — "Mwana wa Mtu atakuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika wake, na hapo ndipo atakapomlipa kila mtu kadiri ya matendo yake."

## SOMO LA 15. YESU ANAWAPENDA WATOTO WADOGO



(Matayo 18:10-14)

**"Jihadharini! Msimdharau mmojawapo wa wadogo hawa. Nawaambieni, malaika wao huko mbinguni wako daima mbele ya Baba yangu aliye mbinguni. (Maana Mwana wa Mtu alikuja kuwaokoa wale waliopotea.) Mnaonaje? Mtu akiwa na kondoo mia, akimpoteza mmoja, hufanyaje? Huwaacha wale tisini na tisa kilimani, huenda kumtafuta yule aliyepotea. Akimpata, nawaambieni kweli, humfurahia huyo zaidi kuliko awafurahiavyo wale tisini na tisa ambao hawakupotea. Hali kadhalika, Baba yenu wa mbinguni hapendi hata mmoja wa hawa wadogo apotee."**

## HADITHI HII INATUFUNDISHA KWAMBA:

1. Watoto wadogo wana malaika. Malaika hawa hutazama uso wa Mungu huko mbinguni. Inafaa tuwe waangalifu jinsi tunavyowatendea watoto. Ni lazima tuwasaidie watoto kutenda yaliyo mema.
2. Jina lingine la Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu. Wakati mwingine huitwa Mwana wa mtu kwa sababu alizaliwa na bikira Maria na mara huitwa Mwana wa Mungu kwa sababu Mungu ni Baba Yake.
3. Kusudi la Yesu kuja hapa ulimwenguni ni kuokoa wapotevu.
4. Yesu anafanana na yule mtu aliyekwenda kumtafuta mwana kondoo aliyepotea, kwa hivyo amekuja kututafuta.
5. Furaha ile yule mtu aliyepata kondoo wake aliyekuwa amepotea alikuwa nayo, ndiyo furaha Yesu huwa nayo mtu mmoja anapomwamini Yeye.
6. Yesu huwa na furaha anapomkuta mpotevu ambaye amekata shauri kumwamini. Hapendi watoto wake wapendwa wapotee, bali anapenda wote waokolewe.
7. Huu ndio umuhimu wa kuwafundisha watoto wetu juu ya Yesu na kuwaongoza kumpenda Yeye.

## JAMBO LA KUFIKIRIA

Swali: Jambo gani linalotendeka kwa mtu anayejaribu kumpotosha mtoto kwa kutomwamini Yesu Kristo?

Jibu: Katika kitabu cha Matayo 18:6 Yesu anasema, "Ye yote atakayemkwaza mmoja wa hawa wadogo wanaoniamini, ingekuwa afadhali afungwe shingoni jiwe kubwa la kusagia na kuzamishwa kwenye kilindi cha bahari."

## YESU ATAKA WATOTO WAJE KWAKE

(Marko 10:13-16)

**Watu walimletea Yesu watoto wadogo ili awaguse, lakini wanafunzi wakawakemea. Yesu alipoona hayo, akakasirika akawaambia, "Waacheni watoto waje kwangu, wala msiwazuie, kwa sababu Utawala wa Mungu ni kwa ajili ya watu walio kama watoto hawa. Nawaambieni kweli, mtu ye yote asiyeupokea Utawala wa Mungu kama mtoto mdogo hatakuwa katika utawala huo." Kisha akawachukua mikononi mwake, akawawekea mikono, akawabariki.**



## SOMO LA 16. NI LAZIMA TUWASAMEHE WENZETU



(Matayo 18:21-25)

**Kisha Petro akamwendea Yesu, akamwuliza, "Je, ndugu yangu akinikosea, nitamsamehe mara ngapi? Mara saba?" Yesu akamjibu, "Sisemi mara saba tu, bali sabini mara saba. Ndiyo maana Utawala wa mbinguni umefanana na mfalme mmoja aliyeamua kukagua hesabu za watumishi wake. Ukaguzi ulipoanza, akaletewa mtu mmoja aliyekuwa na deni la fedha talanta elfu kumi. Mtu huyo hakuwa na cho chote cha kulipa; hivyo bwana wake aliamuru wauzwe, yeye, mke wake, watoto wake na vitu vyote alivyokuwa navyo, ili deni lilipwe. Basi, huyo mtumishi akapiga magoti mbele yake, akasema, 'Unisubiri nami nitakulipa deni lote.' Yule bwana alimwonea huruma, akamsamehe lile deni, akamwacha aende**

zake. Lakini huyo mtumishi akaondoka, akamkuta mmoja wa watumishi wenzake aliyekuwa na deni lake fedha denari mia moja. Akamkamata, akamsonga koo akisema, 'Lipa deni lako!' Huyo mtumishi mwenzake akapiga magoti, akamwomba, 'Unisubiri nami nitakulipa deni lako lote.' Lakini yeye hakutaka, bali alimtia gerezani mpaka hapo atakapolipa lile deni. Basi, watumishi wenzake walipoona jambo hilo walisikitika sana, wakaenda kumpasha habari bwana wao juu ya mambo hayo yaliyotukia. Hapo yule bwana alimwita huyo mtumishi, akamwambia, 'Wewe ni mtumishi mbaya sana! Uliniomba, nami nikakusamehe deni lako lote. Je, haikukupasa nawe kumhurumia mtumishi mwenzako kama nilivyokuhurumia? Basi, huyo bwana alikasirika sana, akamtoa huyo mtumishi aadhibiwe mpaka hapo atakapolipa deni lote. Na Baba yangu aliye mbinguni atawafanyieni vivyo hivyo kama kila mmoja wenu hatamsamehe ndugu yake kwa moyo wake wote."

## HADITHI HII YATUFUNDISHA MAMBO MENGI

1. Msemo huu wa "Sabini mara saba" ni msemo uliotumiwa kuonyesha kwamba msamaha usiwe na mwisho.

2. Mtumishi aliyekuwa na deni la Bwana wake talanta elfu kumi alikuwa na deni kubwa! Mtumishi huyu alikopeshwa shilingi elfu kumi. Ingekuwa vigumu kwake kumlipa mfalme deni hili mara moja.

3. Mtumishi huyu alimwomba mfalme wake kumsubiri kwa muda aendelee kutafuta pesa za kumlipa; mfalme alimpenda mtumishi wake na akamhurumia asilipe deni lile.

4. Mtumishi huyu aliyesamehewa deni lake aliondoka na hakuwa na shukrani kwa tendo hili alilofanyiwa. Naye aliondoka kumdai mdeni wake pesa ndogo alizomkopesha. Alikuwa amemkopesha talanta mia moja tu. Hizi pesa alizomdai mdeni wake hazikuwa nyingi kama zile alizosamehewa na mfal-

me, zilikuwa ndogo sana. Basi alikutana na mdeni wake, akamshika koo na kumlazimisha kumlipa pesa zake mara moja. Mungu huona matendo yetu yote, naye alimwona huyu mtumishi wa kwanza jinsi alivyomtendea mdeni wake; hakumhurumia hata kidogo.

5. Mtumishi huyu wa kwanza hakumsikiliza maskini mdeni wake, isipokuwa alimtupa gerezani mpaka amlipe deni lake. Ikiwa basi yeye mwenyewe alikuwa na shida ya kumlipa mfalme wake deni alilokuwa nalo akiwa huru, je, alifikirije kuhusu kumfunga mdeni wake gerezani na kumlipa? Haingewezekana hata kidogo kumlipa hali yu mfungwa.

6. Mfalme aliambiwa juu ya kisa hiki chote. Mambo haya yalimkasirisha mfalme sana; alifikiri kuhusu huruma aliyomtendea huyu mtumishi wake kwa kumsamehe deni kubwa. Naye alistahili kumsamehe mwenzake!

7. Kwa kuwa huyu mtumishi mwovu hakusamehe, naye vile vile alitupwa gerezani mpaka naye alipe deni alilodaiwa na mfalme.

8. Yesu anasema kwamba jambo hili litafanyika kwetu sisi tusio na huruma na wenzetu au sisi tusio na mioyo ya huruma.

9. Tunasoma Neno la Mungu katika kitabu cha Waroma 3:23 kwamba, "Watu wote wametenda dhambi na wametindikiwa utukufu wa Mungu." Hatungeweza kulipa deni la dhambi zetu mbele za Mungu kwa sababu tulikuwa najisi tusiofaa mbele zake. Isipokuwa Yesu aliyekufa msalabani alistahili mbele za Mungu na ndiye aliyejitoa kufa kwa ajili yetu, ndipo deni zetu zililipwa pale pale. Alikuwa huru

kutoka katika kifungo cha uovu! Katika kitabu cha Yohana wa Kwanza 3:5 tunaambiwa kwamba, "Mnajua kwamba Kristo alikuja kuziondoa dhambi zetu, na kwamba kwake hamna dhambi yo yote."

10. Kwa kuwa Mungu ametusamehe kabisa, naye anataka tuwasamehe wengine wanaotutendea mabaya. Tunapowasamehe wengine tunamwonyesha Mungu kuwa tunamshukuru mioyoni mwetu kwamba naye ametusamehe na kutuweka huru.

### JAMBO LA KUKUMBUKA

Tunakumbushwa kwamba si vizuri kulipiza kisasi kwa mambo mabaya uliyotendewa, isipokuwa kutendeana mema ndilo jambo lililozuri na hilo ndilo jambo zuri ambalo tunastahili kufanya. Bwana Yesu Kristo alisema msilipize kisasi bali mrudishe mema kwa mabaya. Yesu aliwaombea maadui zake hata akawaombea wale waliomtesa. Tunasoma juu ya maombi ya Yesu katika kitabu cha Luka 23:34, "Baba, uwasamehe kwani hawajui wanalofanya."

## SOMO LA 17. TAJIRI WA HUZUNI

(Matayo 19:16-26)



**Mtu mmoja alimjia Yesu, akamwuliza, "Mwalimu, nifanye kitu gani chema ili niupate uzima wa milele?" Yesu akamwambia, "Mbona unaniuliza kuhusu jambo jema? Kuna mmoja tu aliye mwema. Ukitaka kuingia katika uzima shika amri." Yule mtu akamwuliza, "Amri zipi?" Yesu akasema, "Usiue, usizini, usi-**

ibe, usitoe ushahidi wa uongo, waheshimu baba na mama yako; na, mpende jirani yako kama unavyojipenda wewe mwenyewe." Huyo kijana akamwambia, "Hayo yote nimeyazingatia tangu utoto wangu; sasa nifanye nini zaidi? Yesu akamwambia, "Kama unapenda kuwa mkamilifu, nenda ukauze mali yako uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni, kisha njoo ukanifuate." Huyo kijana aliposikia hivyo akaenda zake akiwa na huzuni maana alikuwa na mali nyingi. Hapo Yesu akawaambia wanafunzi wake, "Kweli nawaambieni itakuwa vigumu sana kwa tajiri kuingia katika Utawala wa mbinguni. Tena nawaambieni, ni rahisi zaidi kwa ngamia kupita katika tundu la sindano kuliko kwa tajiri kuingia katika Utawala wa mbinguni." Wale wanafunzi waliposikia hivyo walishangaa, wakamwuliza, "Basi ni nani atakayeweza kuokoka?" Yesu akawatazama, akasema, "Kwa binadamu jambo hili haliwezekani, lakini kwa Mungu kila kitu kinawezekana."

## JAMBO LA KUFANYA

A. Hapa chini kuna nafasi tano ambazo ni wazi, andika maagizo matano ambayo Yesu alimwamuru huyu tajiri kutimiza.

1. ..........................................................................
2. ..........................................................................
3. ..........................................................................
4. ..........................................................................
5. ..........................................................................

B. Jibu maswali yafuatayo na neno NDIYO au LA. Ikiwa jibu ni "ndiyo" andika NDIYO katika nafasi iliyowazi baada ya swali, halafu andika LA ikiwa jibu ni "la."

1. Je, kijana tajiri alisema ameyazingatia maagizo hayo yote? ..............................

2. Je, Yesu alisema kwamba kijana huyo tajiri angeuza vyote alivyokuwa navyo ili awe mkamilifu?

..........................

3. Je, kijana huyu tajiri angeuza mali yake yote na kuwapa matajiri? ......................


4. Je, Yesu alimwuliza huyu kijana tajiri kumfuata? ..........................

5. Je, huyu kijana alimfuata Yesu? ..........................

6. Je, huyu kijana alienda zake akiwa na furaha?

......................

## SOMO LA 18. YESU ATABIRI KWA WANAFUNZI WAKE JINSI ATAKAVYOTENDEWA



(Matayo 20:17-19)

**Yesu alipokuwa anakwenda Yerusalemu, aliwachukua wale wanafunzi kumi na wawili faraghani, na njiani akawaambia, "Sikilizeni! Tunakwenda Yerusalemu na huko Mwana wa Mtu atatolewa kwa makuhani wakuu na walimu wa Sheria. Watamhukumu auawe, watamkabidhi kwa watu wasiomjua Mungu ili adhihakiwe, apigwe viboko na kusulibiwa; lakini siku ya tatu atafufuliwa."**

## KIFO CHA KRISTO HAKIKUWA CHA AJALI

Kabla ya Yesu kuchukuliwa na kusulubishwa msalabani alikuwa amewaeleza wanafunzi wake kuhusu YALE aliyoyatarajia kutendeka kwake. Kifo chake msalabani ulikuwa ni mpango wake wakutuokoa na dhambi zetu. Katika kitabu cha Yohana 3:14, 15, tunaambiwa kwamba, "Kama vile Musa alivyomwinua juu nyoka wa shaba kule jangwani, naye Mwana wa Mtu atainuliwa juu vivyo hivyo, ili kila anayemwamini awe na uzima wa milele." Tunastahili kushukuru kwa haya yote Yesu alitutendea kwa kutufilia. Haithuru hata ikiwa wewe ni nani, warangi gani au mwananchi wa wapi. Jambo la muhimu ni kukumbuka kwamba, ALITUFILIA SISI SOTE. (Soma II Wakorinto 5:15)


Neno **"watu wote"** linamaana **wewe** au **mtu ye yote** atakayeamini! Ukiamini ya kwamba Yesu Kristo alikufa msalabani ili AKUOKOE WEWE kutoka dhambini mwako, basi utakuwa na UZIMA WA MILELE!

**"Maana Mungu aliupenda ulimwengu hivi hata akamtoa Mwanawe wa pekee."**
**— Yohana 3:16a**

## SOMO LA 19. YESU ASHIKWA

(Matayo 27:11-26)

**Yesu alisimamishwa mbele ya mkuu wa mkoa. Basi, mkuu wa mkoa akamwuliza, "Je, wewe ndiwe Mfalme wa Wayahudi?" Yesu akamwambia, "Wewe umesema." Lakini makuhani wakuu na wazee walipokuwa wanamshtaki, hakujibu neno. Hivyo Pilato akamwuliza, "Je, husikii mashtaka hayo yote wanayotoa juu yako?" Lakini Yesu hakumjibu hata neno moja; hata huyo mkuu wa mkoa akashangaa sana. Ilikuwa kawaida wakati wa sikukuu hiyo mkuu wa mkoa kuwafungulia Wayahudi mfungwa mmoja waliyemtaka. Wakati huo kulikuwa na**




mfungwa mmoja, jina lake Baraba. Hivyo, watu walipokusanyika pamoja, Pilato akawauliza, “Mwataka nimfungue yupi kati ya wawili hawa, Baraba ama Yesu aitwaye Kristo?” Alisema hivyo maana alijua wazi kwamba walimleta kwake kwa sababu ya wivu. Pilato alipokuwa amekaa katika kiti cha hukumu, mke wake akampelekea ujumbe: “Usijitie katika shauri la mtu huyu mwema, kwa maana leo nimeteseka sana katika ndoto kwa sababu yake.” Lakini makuhani wakuu na wazee wakawashauri watu waombe Baraba afunguliwe na Yesu auawe. Mkuu wa mkoa akawauliza, “Ni yupi kati ya hawa wawili mnayetaka nimfungue?” Wakamjibu, “Baraba!” Pilato akawauliza, “Sasa, nifanye nini na Yesu aitwaye Kristo?” Wote wakasema, “Asulibiwe!” Pilato akauliza, “Lakini amekosa nini?” Wao wakazidi kupaaza sauti: “Asulibiwe!” Basi, Pilato alipotambua kwamba hafanikiwi cho chote na kwamba maasi yalikuwa yanaanza, alichukua maji, akanawa mikono mbele ya ule umati wa watu, akasema, “Mimi sina lawama juu ya kifo cha mtu huyu; shauri lenu wenyewe.” Watu wote wakasema, “Damu yake na iwe juu yetu na juu ya watoto wetu!” Hapo Pilato akawafungulia Baraba kutoka gerezani, lakini akamtoa Yesu asulibiwe.

## JAMBO LA KUFANYA

Kuna maswali hapa chini utakayoyajibu baada ya kusoma hadithi hii ya 19. Isome hadithi hii tena, na tena halafu uyajibu maswali haya kwa usahihi.

1. Yesu aliposhtakiwa na wakuu makuhani na wazee alijibu nini? ..............................
2. Hii ilimfanya mkuu wa mkoa kushangaa na akasema ..................................
3. Baraba ni jina la mtu aliyejulika kuwa...............
4. Mkuu wa mkoa aliwafungulia mtu gani?............
5. Watu wote walisema Yesu a ...........................

## SOMO LA 20 YESU AVIKWA TAJI YA MIIBA



(Matayo 27:27-30)

**Kisha askari wa mkuu wa mkoa wakamwingiza Yesu ndani ya ikulu, wakamkusanyia kikosi kizima. Wakamvua nguo zake, wakamvika joho la rangi nyekundu, wakasokota taji ya miiba, wakamvika kichwani, wakamwekea pia mwanzi katika mkono wake wa kulia. Wakapiga magoti mbele yake, wakamdhihaki wakisema, "Shikamoo, Mfalme wa Wayahudi!" Wakamtemea mate, wakauchukua ule mwanzi, wakampiga nao kichwani.**

## JINSI KRISTO ALIVYOSULUBIWA

Watu wengi waliokuwa wamejazwa na hasira walimfanyia Yesu mambo mabaya sana. Tukiwa katika


ulimwengu huu twatarajia kuteswa na kufanyiwa mambo mabaya kwa ajili ya Yesu. Watu wakali hawampendi Mungu. Hawampendi Yesu Kristo nao hawapendi wengine ambao wanajaribu kuwapenda. Yesu anatupa mfano wa watu hawa katika Yohana 15:18-20 — "Kama ulimwengu ukiwachukia ninyi, kumbukeni kwamba umenichukia mimi kabla haujawachukia ninyi. Kama mngalikuwa watu wa ulimwengu, ulimwengu ungaliwapenda ninyi, watu wake. Lakini kwa vile ninyi si wa ulimwengu, ila mimi nimewachagueni kutoka ulimwenguni, kwa sababu hiyo ulimwengu unawachukieni. Kumbukeni niliyowaambieni: mtumishi si mkuu zaidi kuliko bwana wake. Ikiwa wamenitesa mimi, watawatesa na ninyi pia." Yesu ana siri ya ajabu anayotaka tuijue na tushirikishwe kwayo. Soma Yohana 16:33, "Nimewaambieni mambo haya ili mpate kuwa na amani katika kuungana nami. Ulimwenguni mtapata masumbuko; lakini jipeni moyo! Mimi nimeushinda ulimwengu!"

## JAMBO LA KUFANYA

Hapa kuna maswali yanayotokana na hadithi ya 20. Isome hadithi hii tena, halafu ujaze na jibu sahihi ukiliandika katika nafasi iliyoachwa wazi.

1. Askari walimvua nguo zake wakamvika ............
2. Walisokota taji ya ................, na walimvika ..........................
3. Walimdhihaki Yesu kwa kumpigia magoti wakisema ..........................
4. Walipomaliza kumdhihaki walim .......... .........., na ........................ kichwani.

# SOMO LA 21. YESU ASULUBISHWA




(Matayo 27:31-38 na 50-54)

**Walipomaliza kumdhihaki wakamvua lile joho, wakamvika mavazi yake kisha wakampeleka kumsulibisha. Walipokuwa wakienda, wakamkuta mtu mmoja jina lake Simoni, mwenyeji wa Kurene, wakamlazimisha kuuchukua msalaba wake Yesu. Walipofika mahali paitwapo Golgotha, maana yake, "Fuvu la kichwa," wakampa mchanganyiko wa divai na nyongo. Lakini Yesu alipoonja akakataa kunywa. Walimsulibisha, kisha wakagawana mavazi yake kwa kuyapigia kura. Wakaketi, wakawa wanamchunga. Juu ya kichwa chake wakaweka mshtaka wake ulioandikwa, "Huyu ni Yesu Mfalme wa Wayahudi." Wanyang'anyi wawili walisulibiwa pia pamoja naye, mmoja upande wa kushoto na mwingine upande wa kulia. Basi, Yesu akalia tena kwa sauti kubwa, akakata roho. Hapo pazia la Hekalu likapasuka vipande viwili, toka juu mpaka chini; nchi ikatetemeka; mawe yakapasuka; makaburi yakafunguliwa na watu wengi wa Mungu waliokufa wakafufuliwa; nao, baada ya kufufuka kwake, wakatoka makaburini, wakaingia katika mji mtakatifu, wakaonekana na watu wengi. Basi, jemadari na wale waliokuwa wakimchunga Yesu walipoona mtetemeko wa nchi na yale mambo yaliyotukia, wakaogopa sana, wakasema, "Hakika mtu huyu alikuwa Mwana wa Mungu."**

ALIKUWA NANI?

1. Ni nani aliyelazimishwa kuubeba msalaba wa Yesu? ......................

2. Yesu alisulubishwa na watu gani ambao mmoja alikuwa kwa mkono wa kulia na mwingine mkono wa kushoto? ......................................

3. Wakati jemadari na watu wengine waliokuwa wakimchunga Yesu walipoona mtetemeko wa nchi na mambo mengine yaliyotendeka walisema kuwa Yesu alikuwa nani? ......................................

## SOMO LA 22. YESU AZIKWA



(Matayo 27:57-66)

**Ilipokuwa jioni, akaja mtu mmoja tajiri mwenyeji wa Arimataya jina lake Yosefu. Yeye pia alikuwa mwanafunzi wa Yesu. Akamwendea Pilato akaomba apewe mwili wa Yesu. Basi, Pilato akaamuru apewe. Yosefu akauchukua ule mwili akauvika sanda safi, akauweka ndani ya kaburi lake jipya alilokuwa amelichonga katika mwamba. Kisha akavingirishia jiwe kubwa mbele ya mlango wa kaburi, akaenda zake. Maria Magdalene na yule Maria mwingine walikuwa wameketi kulielekea kaburi. Kesho yake, yaani siku iliyofuata ile ya Maandalio, makuhani wakuu na Wafarisayo walimwendea Pilato wakasema, "Mheshimiwa, tunakumbuka kwamba yule mdanganyifu alisema kabla ya kufa ati, 'Baada ya siku tatu nitafufuka'. Kwa hiyo amuru kaburi lilindwe mpaka siku ya tatu ili wanafunzi wake wasije wakamwiba na kuwaambia watu kwamba amefufuka. Uwongo huu wa mwisho uta-**

kuwa mbaya zaidi kuliko ule wa awali." Pilato akawaambia, "Haya, mnao walinzi, nendeni mkalinde kadiri mjuavyo." Basi, wakaenda, wakalilinda kaburi, wakatia muhuri juu ya lile jiwe na kumwacha hapo askari mlinzi.

## YOSEFU ALIMPENDA YESU

Yosefu alikuwa tajiri, alimpenda Yesu, naye alitaka kumzika Yesu katika kaburi lake. Yosefu alikuwa amepanga kuzikwa kwa kaburi lile lake atakapokufa; lakini, alibadili nia yake na kukata shauri kwamba mpendwa wake Yesu Kristo apumzike katika kaburi lake lililokuwa zuri. Upendo hutumika. Wampenda Yesu? Je, umejaribu kumtumikia? Unamfanyia nini?

## YESU ALIYATOA MAISHA YAKE

Kwa kupenda kwake alitoa maisha yake kuniokoa mimi na wewe kutoka dhambini. Kifo chake na kumwagika kwa damu yake isiyo na hatia ilikuwa ni sadaka ya kuchukua dhambi zetu. Katika kitabu cha Waebrania 9:22 tunasoma kwamba Yesu asingalimwaga damu yake hatungekuwa na ondoleo la dhambi. Yesu alikuwa kafara wa kweli kwa sababu hakuwa na dhambi zo zote. Katika Yohana 1:29 tunaambiwa kwamba, "Huyu ndiye Mwana-kondoo wa Mungu aondoaye dhambi ya ulimwengu!" Hakuna mtu mwingine ambaye angekufa msalabani ili kuziondoa dhambi zetu, tena hakuna kitu cho chote kama fedha au zahabu au ng'ombe au mnyama ye yote au kiumbe cho chote kiishicho kingekuwa ondoleo la dhambi. Soma I Petro 1:18-19: "Maana mnajua kwamba ninyi mlikombolewa katika mwenendo wenu usiofaa ambao mliupokea kutoka kwa wazee wenu, si kwa vitu vyenye kuharibika: kwa fedha na dhahabu; bali mlikombolewa kwa damu tukufu ya Kristo, am-

baye alikuwa kama mwana-kondoo asiye na dosari wala doa."

Tunajua kwamba Yesu alitoa maisha yake bure. Katika kitabu cha Yohana 10:18 tunasoma kwamba: "Hakuna mtu anayeninyang'anya maisha yangu; mimi nayatoa kwa hiari yangu mwenyewe. Ninao uwezo wa kuyatoa na uwezo wa kuyachukua tena. Hivi ndivyo Baba alivyoniamuru kufanya." YESU ANA UWEZO WOTE! Tena Matayo 28:18.

Yesu aliposimama mbele ya Pilato kuhukumiwa, Pilato alidhani kwamba alikuwa na uwezo wa kumsamehe au kumsulubisha Yesu. Ninataka uone maneno ya Yesu, soma Yohana 19:11, "Yesu akamjibu, Hungekuwa na mamlaka yo yote juu yangu kama hungepewa na Mungu."

Kristo alitoa maisha yake kwa watu wote wa mataifa yote ili kwamba wote wamwamini Yesu Kristo na kuokolewa. Ni heri uhakikishe kwamba WEWE ni mmoja wa wale wanao MWAMINI BWANA YESU! Soma Ufunuo 5:9, "Basi, wakaimba wimbo huu mpya, Wewe unastahili kukitwaa hicho kitabu na kuivunja mihuri yake. Kwa sababu wewe umechinjwa, na kwa damu yako umemnunulia Mungu watu kutoka katika kila kabila, lugha, jamaa na taifa."

## ADUI ZAKE WALIJARIBU KUONA KWAMBA YESU ASIIBIWE KUTOKA KABURINI

Makuhani na Mafarisayo ambao walikuwa ni maadui wa Yesu walitaka kuhakikisha kwamba kaburi lake lilifungwa vizuri kwamba mtu asije kuuiba mwili wake. Jambo hili linafanya kufufuka kwa Yesu kuwa kwa ajabu, tukifahamu kwamba haingewezekana kwa wale walioshuhudia kisa hicho kwamba mwili wake

ungeweza kuibwa! Hata tunasoma kwamba waliwaweka walinzi kulinda kaburi hilo. Tutaona maajabu yaliyotendeka hapo tutakaposoma Hadithi ya 23.

## MIKONO ILIYOHARIBIWA

"Kwa nini mnaiadhimisha siku ya kusulubishwa kwa Yesu?" Niliulizwa swali hili na mtu mmoja aliyefikiri kwamba halikuwa jambo zuri; kwa maoni yake lilikuwa ni jambo la kutisha. Aliniambia, "Fikiri juu ya kuazimisha kwa siku kuu ya Warumi, kwamba kwa vyo vyote, mtu kufa lilikuwa ni jambo la kuhuzunisha. Msalaba ulilazwa chini, kafara au mhanga aliwekwa juu yake, alichomwa au kupigiliwa na misumari mikubwa katika mikono na miguuni ili asitoke, halafu msalaba uliinuliwa na kutumbukizwa kwa shimo lililochimbwa na kafara aliyetundikwa juu hutungika mpaka afe. Na hili ndilo jambo Wakristo husherehekea katika siku ya kufa kwa Yesu! Ninasikitika kwamba hili si jambo zuri, ni jambo la kuogofya, sioni jinsi inavyowezekana kufanya hivyo."

Nikamjibu, "Rafiki yangu, unafikiria tendo hili bila kufikiri maana ya Yesu kutundikwa msalabani na kuteswa. Hujalinganisha tendo hili na yule aliyetendewa. Hebu nikuambie hadithi moja niliyosikia.

"Kulikuwa na mwanamke mmoja aliyekuwa mrembo, lakini mikono yake ilikuwa imeharibika sana. Huyu mrembo alikuwa na mtoto, huyu mtoto wake alikuwa akijiuliza juu ya sababu zilizomfanya mama yake kuharibika mikono. Mtoto huyu alichukia kuona mikono ya mama yake. Siku moja alimwuliza mamaye, " 'Mama, napenda uso wako, macho yako na nywele zako. Hivi vyaonekana vizuri sana; lakini mama, mikono yako—ni mibaya sana, siipendi na sipendi

kuiangalia. Kwa nini imejikunjakunja na kuwa na makovu makovu jinsi hii?'

" 'Nisikilize mwanangu; sikutaka kukuambia, lakini naona kwamba heri ujue kwa nini mikono yangu iko hivi. Sasa ni kama miaka kumi iliyopita. Ulikuwa mtoto mdogo wakati ule—nilikupenda sana, lakini sikukupenda jinsi ninavyokupenda sasa. Wakati ule ulikuwa na miezi mitatu, asubuhi moja tulikuwa tukishughulika. Nilikuwa nimekulisha na kukulaza kitandani mwako ili ulale; nilienda kufanya kazi yangu jikoni na huku nikitega sikio kukusikiliza kama ungeamka na kulia nije kukuchukua. Nilikaa kwa muda mfupi tu, haukuwa muda mrefu.

" 'Kwa ghafula niliitwa. Nilipoangalia nje, niliwaona jirani zangu wakikimbia kuelekea kwa nyumba yetu wakisema, moto! moto! Nilitoka jikoni mbio nikaona nyumba yetu inaungua, mle wewe ulimokuwa umelala; moto ulikuwa umeishika nyumba nzima. Majirani walikuja kunisaidia. Nilishindwa nalakufanya, nilibaki nimepumbaa na kupanua mdomo tu, sikuweza kusema neno lo lote. Kulikuwa na shali kubwa karibu na mahali niliposimama, nilichukua na kujifunika kichwani na nikaacha mikono wazi, niliingia nyumbani mahali ulipokuwa. Sikujali moto, nilikuchukua na kukufunga katika shuka ya kitanda na kukukumbatia kifuani na nikatoka nawe nje. Mikono yangu ilichomeka hata nyama zikaanguka na ikabaki mifupa hivi. Hii ndiyo hadithi ya mikono yangu kuharibika hivi.'

"Waonaje kuhusu msichana huyu? Alikuwa mtoto wa kawaida. Alijiona kuwa ana sura yake ya kawaida, hakuona kasoro yo yote juu yake. Kwa huruma na

upendo alishika mikono ya mama yake akaibusu akamwangalia mama yake, akasema: 'O! Mama nakupenda, napenda uso wako, macho yako, shingo lako, nywele zako, lakini mikono hii naipenda mno!' Kwa hivyo tufikiri kuhusu kifo cha Yesu pale msalabani." — Presbyterian Banner

## WAJIBU WETU KWA MUNGU

1. Tutubu dhambi zetu kwa Kristo ili tusamehewe. (I Yohana 1:9)
2. Tuamini Yesu Kristo kwa kuokolewa. (Matendo 16:31)
3. Tumpende Mungu wetu kwa roho, yetu, na kwa mawazo yetu yote. (Matayo 22:37)
4. Ni lazima tumkiri Kristo kuwa Mwana wa Mungu. (Matayo 10:32)
5. Tuishi maisha ya kumpendeza Mungu. (I Watesalonike 4:1)

## SOMO LA 23. YESU AFUFUKA KUTOKA KWA WAFU

(Matayo 28:1-10)



**Baada ya Sabato, karibu na mapambazuko ya siku ile ya Jumapili, Maria Magdalena na yule Maria mwingine walikwenda kutazama lile kaburi. Ghafula kukatokea mtetemeko mkubwa wa nchi; malaika wa Bwana alishuka kutoka mbinguni, akaliondoa lile jiwe, akaketi juu yake. Kuonekana kwake kulikuwa kama umeme na mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji.**

**Walinzi wa lile kaburi wakatetemeka kwa hofu kubwa, hata wakawa kama wamekufa. Lakini yule malaika akawaambia wale wanawake, "Ninyi msiogope! Najua kwamba mnamtafuta Yesu aliyesulibiwa. Hayupo hapa maana amefufuka kama alivyosema. Njooni mkaone mahali alipokuwa amelala. Basi, nendeni upesi mkawaambie wanafunzi wake kwamba amefufuka katika wafu, na sasa anawatangulieni kule Galilaya; huko mtamwona. Haya, mimi nimekwisha waambieni." Wakiwa wenye hofu na furaha kubwa, hao wanawake walitoka upesi kaburini, wakakimbia kwenda kuwaambia wanafunzi wake. Mara, Yesu akakutana nao, akawaamkia: "Salamu." Hao wanawake wakamwendea, wakapiga magoti mbele yake wakashika miguu yake. Kisha Yesu akawaambia, "Msiogope! Nendeni mkawaambie ndugu zangu waende Galilaya na huko wataniona."**

### JAMBO LA KUFANYA

Soma hadithi hii ya 23 na ujaze katika nafasi zilizowazi na neno lililosawa.

1. Malaika wa Bwana alishuka kutoka mbinguni akaliondoa .......................... Mavazi yake yalikuwa meupe kama ..................................
2. Walinzi waliogopa na kutetemeka kama ..........

YESU ALISHINDA kifo, jehanam, na kaburi ili kwamba tuishi tena! Katika kitabu cha Yohana 14:19 Anasema: "Kwa kuwa mimi ni hai, nanyi pia mtakuwa hai." Katika Yohana 11:25-26 Anasema: "Mimi ndimi ufufuko na uzima. Anayeniamini mimi hata kama anakufa ataishi; na kila anayeishi na kuniamini hatakufa kamwe."

## SOMO LA 24. MANENO YA MWISHO YA YESU

(Matayo 28:16-20)

**Wale wanafunzi kumi na mmoja walikwenda Galilaya kwenye ule mlima aliowaagizia Yesu. Walipomwona wakamwabudu, ingawa wengine walikuwa na mashaka. Yesu**

**akaja karibu akawaambia, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Nendeni, basi, mkawafanye watu wa mataifa yote wawe wafuasi; wabatizeni kwa jina la baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Wafundisheni kushika maagizo yote niliyowapeni. Nami nipo pamoja nanyi siku zote; naam, mpaka mwisho wa nyakati."**

Rafiki yetu mpendwa anapokufa sisi hupenda kuwaambia watu wengine maneno yake ya mwisho. Maneno yake ya mwisho hukaa katika mawazo yetu. Tunajua kwamba maneno ambayo mtu anayekufa anasema ni ya maana sana! Maneno ya Bwana wetu Yesu aliyoyasema kabla ya kwenda mbinguni ni haya, "Nendeni ulimwenguni kote mkahubiri Habari Njema kwa kila mtu." (Marko 16:15)

Je, unajaribu kutimiza maneno haya ya Yesu?

## KWA NINI TUWAAMBIE WENGINE?

Tunasoma katika kitabu cha Matendo 4:12 kwamba, "Wokovu haupatikani kwa mtu mwingine ye yote, kwa maana duniani pote, binadamu hawakupewa jina la mtu mwingine ambaye sisi tunaweza kuokolewa naye." Hii inatuonyesha kwamba YESU tu ndiye TUMAINI letu la Uzima wa Milele!

Katika Yohana 14:6 tunaona jibu la Yesu, alimjibu hivi: "Mimi ni njia, ukweli na uzima. Hakuna awezaye kwenda kwa Baba ila kwa kupitia kwangu." Pia twaona kwamba YESU ndiye NJIA ya pekee kwenda kwa BABA!

## UCHUNGUZI WA KUTAMBUA MFASI WA KWELI WA KRISTO

Yesu anasema kwamba, "Mkinipenda mtazishika amri zangu." (Yohana 14:15) Amri kuu na ya kwanza iko katika kitabu cha Matayo 22:37. Inasema kuhusu

wajibu wetu na Mungu. Amri yenyewe ndiyo hii: "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote na kwa akili zako zote." Amri kuu ya pili inahusu wajibu wetu na watu wote po pote ulimwenguni. Amri hii inapatikana katika kitabu cha Matayo 22:39. Inasema: "Mpende jirani yako kama unavyojipenda wewe mwenyewe!" Unabii wote na sheria zote viko katika sheria hizi mbili. (Soma Matayo 22:40)

## SOMO LA 25. YESU ATAKUJA DUNIANI TENA

### ISHARA ZA KUJA KWAKE YESU NI ZIPI?

Ili upate kielelezo kizuri cha kuja kwake Kristo, kwanza soma mlango wa Matayo 24. Pia tumetaja hapa chini kuhusu mambo yatakayotendeka.

1. Wakristo wengi wa udanganyifu watatokea nao watasema wao ndiye Kristo, watawadanganya wengi. Msiwafuate. (Mistari 5, 23, 24 and 25)
2. Kutakuwa na vita na uvumi wa mapigano ya utawala mmoja ukipigana na mwingine, taifa moja litapigana na lingine. (Mstari wa 7)
3. Kutakuwa na njaa hapa na pale na mitetemeko ya nchi. Yote haya ni mwanzo wa huzuni. (Mistari 7, 8)
4. Wakristo watatolewa na kuteswa, kuuawa na kuchukiwa na mataifa yote kwa ajili ya Jina la Kristo. (Mstari wa 9) Yesu alikuja hapa ulimwenguni kuteswa kwa ajili yetu, ili tuwe na uzima wa milele, ndipo tutakapohakikisha upendo wetu kwake kwa kuteswa kwa ajili yake.
5. Wakristo wengi wataanza kufifia na kuacha kumfuata Kristo, watasengenyana na kusalitiana na

kuchukiana. (Mstari wa 10)

6. Manabii wengi wa uwongo watatokea, watawadanganya watu wengi. Watakuwa na nguvu na uwezo wa kufanya maajabu na miugiza wakidanganya hata na Wakristo wema. (Mistari 11 na 24)

7. Kutakuwa na kula na kunywa kwa wingi, watu wataoa na kuolewa kama zile siku za Noa alipoishi hapa duniani. (Mistari 37-39)

8. Baada ya dhiki na maumivu makuu, jua litatiwa giza, mwezi hautatoa mwangaza, nazo nyote za mbinguni zitaanguka na nguvu za mbinguni zitatikiswa! (Mstari wa 29)

## YESU ATAKUJA KWA NJIA GANI?

1. Kuja kwake kutakuwa kwa ghafula. Katika Matayo 24:27 twasoma:"Kama vile umeme uangazavyo kutoka mashariki hadi magharibi, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Mtu."

2. Atakuja juu ya mawingu ya angani, mwenye nguvu na utukufu wingi. (Matayo 24:30)

3. Na katika Ufunuo 1:7 tunajulishwa kwamba, ". . . kila mtu atamwona."


4. "Maana patatolewa amri, sauti ya malaika mkuu, sauti ya tarumbeta ya Mungu, naye Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni. Ndipo wale waliokufa wakiwa wanamwamini Kristo watafufuliwa kwanza. Kishi sisi tulio hai wakati huo tutakusanywa pamoja nao katika mawingu kumlaki Bwana hewani. Na hivyo tutakuwa daima pamoja na Bwana. Basi, farijianeni kwa maneno haya." (I Watesalonike 4:16-18)

5. ". . . Yesu huyu ambaye amechukuliwa kutoka kwenu kwenda mbinguni atakuja tena namna hiyo

hiyo mlivyomwona akienda mbinguni." (Matendo 1:11)

## JINSI YA KUJIWEKA TAYARI KWA YESU

"Lakini tukiishi katika mwanga, kama naye alivyo katika mwanga, basi, tutakuwa na umoja sisi kwa sisi, na damu yake Yesu Kristo, Mwanae, inatutakasa dhambi zote." — I Yohana 1:7





Zaburi 86:5 — "Wewe, Bwana, U mwema, umekuwa tayari kusamehe, na mwingi wa fadhili, kwa watu wote wakuitao."

Yohana 14:6 — "Yesu akamjibu (Toma), Mimi ni njia, ukweli na uzima. Hakuna awezaye kwenda kwa Baba ila kwa kupitia kwangu."

## JINSI YA KUFIKA HUKO

### HATUA YA 1 — SIKITIKIA DHAMBI ZAKO ZOTE

Msichana mmoja mdogo aliniambia kwamba, "Kusikitikia dhambi zako inamaana kwamba usikitike sana na kuziacha kabisa."




Shetani hutumia tabia mbaya kwa kuwafunga watu dhambini.

Anatufunga na minyororo ili tusiwe huru.


Njoo na minyororo hiyo kwa Yesu naye atakuweka huru.

### HATUA YA 2 — KUTUBU NA KUMKIRI MUNGU

I Yohana 1:9 — "Tukiziungama dhambi zetu, basi, Mungu ni mwaminifu na mwadilifu, naye atatusamehe dhambi zetu na kututakasa na uovu wote."

**MWAMBIE YESU YOTE — YEYE ASIKIA MAOMBI YAKO**

Fatisha kwa kuunganisha ili ugundue jina la yule awezaye kuvunja minyororo ya dhambi.



**HATUA YA 3 — MWAMINI NA KUMKUBALI MOYONI NA MAISHANI MWAKO**

Fungua mlango wa moyo wako na umruhusu Yesu kuingia na kukaa SASA HIVI!!

Ufunuo 3:20 — "Sikiliza! Mimi nasimama mlangoni na kubisha hodi. Mtu akisikia sauti yangu na kufungua mlango, nitaingia nyumbani kwake na kula chakula pamoja naye, naye atakula pamoja nami."

Tutapata tumaini la kweli kwamba sisi ni mali yake tutakapotubu dhambi na kumwamini.

Waroma 8:16 — "Naye Roho mwenyewe anajiunga na roho zetu na kuthibitisha kwamba sisi ni watoto wa Mungu."

**JE, UMEMWAMINI Bwana Yesu Kristo kuwa Mwokozi wako?**

**KUTIMIZA NENO LA MUNGU**

1. **Tukisha** tubu dhambi zetu

na

2. **Tukisha** mwamini Bwana Yesu Kristo kuwa **MWOKOZI WETU.**

3. **Ndipo, — tutakapotimiza Neno la Mungu.**

Ni lazima tuendelee kuishi katika mwanga na kumfuata Yesu wakati wa maisha yetu ya **kila siku.** Usome I Yohana, mlango 1, mstari wa 7.


## HATUA YA 4 — ENDELEA KUMWISHIA KRISTO

Soma Yohana 8:31-32 — ". . . Kama **mkiyazingatia mafundisho** yangu **mtakuwa kweli wanafunzi wangu.** Mtaujua ukweli, nao ukweli, utawapeni uhuru."

## UKIMWOMBA MUNGU KILA SIKU UTAKUWA NA NGUVU

JAMBO LA KUFANYA

Ipake mikono hii rangi ukionyesha jambo tunalostahili kufanya ili tukue na nguvu katika Mungu wetu.




## SOMA NENO LA MUNGU KILA SIKU

Ufiche Neno la Mungu ndani ya moyo wako. Jifunze kwa moyo maandiko matakatifu jinsi unavyoweza.

## JE, UMEMPOKEA KRISTO KUWA MWOKOZI WAKO?

Ikiwa umempokea Yesu moyoni mwako andika jina lako kwenye mistari iliyoko kwenye picha hii ya moyo.



WAAMBIE WENGINE JUU YA YESU NA YALE ALIYOKUTENDEA.

## MUNGU ALIUUMBA ULIMWENGU WETU



(Mwanzo 1:1-25)

Hapo mwanzo Mungu alizi-umba mbingu na nchi. Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utu-pu, na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji; Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji. Mungu akasema, Iwe nuru; ikawa nuru. Mungu akaiona nuru, ya kuwa ni njema; Mungu akatenga nuru na giza. Mungu akaiita nuru Mchana, na giza akaliita Usi-ku. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku moja.

Mungu akasema, Na liwe anga katikati ya maji, likaya-tenge maji na maji. Mungu akalifanya anga, akayatenga yale maji yaliyo juu ya anga na yale maji yaliyo chini ya anga; ikawa hivyo. Mungu akaliita lile anga Mbingu. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya pili.

Mungu akasema, Maji yali-yo chini ya mbingu na yaku-sanyike mahali pamoja, ili pakavu paonekane; ikawa hi-vyo. Mungu akapaita pale pakavu Nchi; na makusanyiko ya maji akayaita Bahari; Mu-ngu akaona ya kuwa ni vyema. Mungu akasema, Nchi na itoe majani, mche utoao mbe-gu, na mti wa matunda uzaao matunda kwa jinsi yake, am-bao mbegu zake zimo ndani yake, juu ya nchi; ikawa hi-vyo. Nchi ikatoa majani, mche utoao mbegu kwa jinsi yake, na mti uzaao matunda, ambao mbegu zake zimo nda-ni yake, kwa jinsi yake; Mu-ngu akaona ya kuwa ni vyema. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya tatu.

Mungu akasema, Na iwe mianga katika anga la mbingu ili itenge kati ya mchana na usiku; nayo iwe ndiyo dalili na majira na siku na miaka; tena iwe ndiyo mianga katika anga la mbingu itie nuru juu ya nchi; ikawa hivyo. Mungu

akafanya mianga miwili mikubwa, ule mkubwa utawale mchana, na ule mdogo utawale usiku; akafanya na nyota pia. Mungu akaiweka katika anga la mbingu, itie nuru juu ya nchi na kuutawala mchana na usiku na kutenga nuru na giza; Mungu akaona ya kuwa ni vyema. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya nne.

Mungu akasema, Maji na yajawe kwa wingi na kitu kiendacho chenye uhai, na ndege waruke juu ya nchi katika anga la mbingu. Mungu akaumba nyangumi wakubwa, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho, ambavyo maji yalijawa navyo kwa wingi kwa jinsi zao, na kila ndege arukaye, kwa jinsi yake; Mungu akaona ya kuwa ni vyema. Mungu akavibarikia, akisema, Zaeni, mkaongezeke, mkayajaze maji ya baharini, ndege na wazidi katika nchi. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya tano.

Mungu akasema, Nchi na izae kiumbe hai kwa jinsi zake, mnyama wa kufugwa, nacho kitambaacho, na wanyama wa mwitu kwa jinsi zake; ikawa hivyo. Mungu akafanya mnyama wa mwitu kwa jinsi zake, na mnyama wa kufugwa kwa jinsi zake, na kila kitu kitambaacho juu ya nchi kwa jinsi yake; Mungu akaona ya kuwa ni vyema.

## MUNGU ALIMWUMBA MWANADAMU

(Mwanzo 1:26-31)

Mungu akasema, Na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi. Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwa-



umba. Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi. Mungu akasema, Tazama, nimewapa kila mche utoao mbegu, ulio juu ya uso wa nchi yote pia, na kila mti, ambao matunda yake yana mbegu; vitakuwa ndivyo chakula chenu; na chakula cha kila mnyama wa nchi, na cha kila ndege wa angani, na cha kila kitu



**kitambaacho juu ya nchi, chenye uhai; majani yote ya miche, ndiyo chakula chenu; ikawa hivyo. Mungu akaona kila kitu alichokifanya, na tazama, ni chema sana. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya sita.**

(Mwanzo 2:7)

**BWANA Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai.**

## JAMBO LA KUKUMBUKA

Mtu ameumbwa tofauti na wanyama wengine. Sisi si kama wanyama wa mwituni. Tunaambiwa na Biblia kwamba, "Miili ya viumbe vyote si sawa. Miili ya binadamu ni ya namna moja, ya wanyama ni ya namna nyingine, ya ndege ni ya namna nyingine na miili ya samaki pia ni ya namna nyingine." (I Wakorinto 15:39) Mwili na moyo wa mtu vimeumbwa tofauti na wanyama wengine. Roho ya mtu inaishi. Tangu kuzaliwa na hata kufa, roho ya mtu huwa mahali fulani. Watu wanaomwamini Bwana Yesu Kristo kuwa Mwokozi wao watakuwa na uzima wa milele, lakini wale ambao hawamwamini watahukumiwa milele. Katika kitabu cha Yohana 5:28-29 tunasoma kwamba, "Msistaajabie jambo hili; maana wakati unakuja ambapo wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake, nao watafufuka: wale waliotenda mema watafufuka na kuishi, na wale waliotenda maovu watafufuka na kuhukumiwa."

Sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo. Waebrania 9:27 tunasoma kwamba, "Basi,

kama vile kila mtu hufa mara moja tu, kisha husimama mbele ya hukumu ya Mungu." Waroma 14:10-12 Biblia inasema kwamba, "... Sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu. Maana Maandiko yanasema: Kama niishivyo, asema Bwana, kila mtu atanipigia magoti; na kila mmoja atakiri kwamba mimi ni Mungu. Kwa hiyo, kila mmoja wetu atatoa hoja yake mbele ya Mungu."

Kifungu hiki kilichoandikwa hapa juu chatuonyesha kwamba sisi ni tofauti na wanyama wengine. Ni kweli kwamba wanyama hufa nao hurudi mchangani kuwa vumbi, lakini kitabu cha Mhubiri 3:21 kinatuonyesha utofauti kati ya roho ya mtu na roho ya mnyama. Kinasema hivi, "Ni nani ajuaye kama roho ya binadamu huenda juu, na kama roho ya mnyama huenda chini?"

Kwa hivyo, tumesoma kwamba roho ya mtu hurudi kwa Mungu aliyeiumba. Mhubiri 12:7 tunasoma hivi, "Nayo mavumbi kuirudia nchi kama yalivyokuwa, nayo roho kumrudia Mungu aliyeitoa."

## MWANADAMU ANAHITAJI MWOKOZI

Waroma 3:23 — "Watu wote wametenda dhambi na wametindikiwa utukufu wa Mungu."

Waroma 5:12 — "Kwa njia ya mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, nayo ikasababisha kifo. Hivyo kifo kimeenea katika jumuiya yote ya binadamu, kwa maana wote wametenda dhambi."

Yohana 3:5 — "Mtu asipozaliwa kwa maji na Roho, hawezi kamwe kuingia katika Utawala wa Mungu."

## MUNGU ALIMTOA MWOKOZI

Waroma 5:6-11 — "Tulipokuwa bado wanyonge,

Kristo, wakati maalum, alikufa kwa ajili yetu sisi waovu. Si rahisi mtu kufa kwa ajili ya mtu mwadilifu; labda mtu anaweza kuthubutu kufa kwa ajili ya mtu mwema. Lakini Mungu amethibitisha kwamba anatupenda, maana wakati tulipokuwa bado wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu. Kwa kuwa sasa tumefanywa kuwa wenye uhusiano mwema na Mungu kwa kifo cha Kristo, ni dhahiri zaidi kwamba atatuokoa katika ghadhabu ya Mungu. Maana, tulipokuwa bado adui zake, Mungu alitupatanisha naye kwa kifo cha Mwanae. Na kwa vile sasa tumepatanishwa naye, ni dhahiri zaidi kwamba tutaokolewa kwa uzima wa Kristo. Wala si hayo tu, ila tunafurahi pia katika Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo ambaye ametupatanisha na Mungu."

Yohana 3:16-17 — "Maana Mungu aliupenda ulimwengu hivi hata akamtoa Mwanae wa pekee, ili kila anayemwamini asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma Mwanae ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali aukomboe ulimwengu."

## ILI TUOKOLEWE NI LAZIMA TUMWAMINI KRISTO

Yohana 3:18 — "Anayemwamini Mwana hahukumiwi; asiyemwamini amekwisha hukumiwa kwa sababu hakumwamini Mwana wa pekee wa Mungu."

Matendo 16:31 — "Mwamini Bwana Yesu nawe utaokolewa pamoja na jamaa yako yote."

Yohana 5:24 — "Anayesikia neno langu, na kumwamini yule aliyenituma anao uzima wa milele. Hatahukumiwa kamwe, bali amekwisha pita kutoka kifo na kuingia katika uzima."

Majibu ya maswali ya toleo hili la kitabu cha Matayo tunachoita "Furaha" yanapatikana hapa chini. Unaweza kulinganisha jibu lako uone kama ulipata sawa. Unaweza kuangalia jibu lako baada ya kujaribu kwanza. Ikiwa utakosa tatu au chini ya tatu, ujue umefanya kazi nzuri sana.

**Ukurasa 1, 2**

A. 1. Maria
2. Roho Mtakatifu
3. Malaika
4. Mungu pamoja nasi

**Ukurasa 5**

A. 1. Ndiyo 4. La
2. Ndiyo 5. Ndiyo
3. La 6. Ndiyo

B. Wakaingia nyumbani, wakamwona yule mtoto pamoja na **Maria** mama yake; wakapiga magoti, wakamsujudia. Kisha wakafungua hazina zao, wakampa **zawadi: dhahabu**, ubani na **manemane.**

**Ukurasa 8**

A. 1. Mbinguni 3. Yesu
2. Nzige na asali 4. Njiwa
5. Mwanangu

**Ukurasa 10**

A. 1. Arobaini 3. Hekalu
2. Ibilisi (majaribu au Shetani) 4. Mkate
5. Kumsujudia yeye

**Ukurasa 13**

A. 1. Andrea 3. Yohana
2. Wavu

**Ukurasa 15, 16**

A. Baba yetu uliye **mbinguni:** jina lako litukuzwe, Utawala wako ufike, Utakalo lifanyike **duniani** kama **mbinguni**. Utupe leo **chakula** chetu tunachohitaji; Utusamehe makosa yetu kama nasi tunavyowasamehe **waliotukosea;** Usitutie katika majaribu, lakini utuokoe na yule **Mwovu.**

**Ukurasa 21**

A. 1. Mtu mwenye busara
2. Mtu mpumbavu

**Ukurasa 27, 28**

A. 1. Ndege
2. Mchanga, —nyauka, —kauka

B. 1. Neno, —elewa neno
2. Neno, huanguka
3. Ulimwengu, matunda

**Ukurasa 37, 38**

A. 1. Usiue
2. Usizini
3. Usiibe
4. Usimshuhudie jirani uwongo
5. Heshimu baba na mama yako
6. Mpende jirani yako kama nafsi yako

B. 1. Ndiyo 4. Ndiyo
2. Ndiyo 5. La
3. La 6. La

**Ukurasa 41**

A. 1. Lo lote 4. Baraba
2. Sana 5. —sulibiwe
3. Mfungwa

**Ukurasa 42**

A. 1. Joho la rangi nyekundu
2. Miiba, kichwani
3. Mfalme
4. -temea mate, walimpiga

**Ukurasa 44**

A. 1. Simoni Mkrene
2. Wanyang'anyi
3. Mwana wa Mungu

**Ukurasa 50**

A. 1. Jiwe, theluji
2. Wafu

## JAMBO LA KUFANYA

Katika nafasi zilizoachwa wazi andika “NDIYO” kando ya swali ikiwa unasema ukweli.

_______1. Uliposoma kitabu hiki cha “FURAHA” ulisikia Mungu akizungumza na moyo wako?

_______2. Je, unataka kuwa mfasi wa Yesu na kupata UZIMA WA MILELE?

_______3. Je, umesikitikia mambo yote mabaya uliyoyatenda? Je, unahitaji kutubu dhambi zako na kuziacha kabisa?

_______4. Umemwomba Yesu na kumwambia kwamba umesikitika?

_______5. Je, umemwomba Yesu rohoni mwako na kupata hakikisho kwamba amesikia maombi yako na amekusamehe dhambi zako zote? Kumbuka kwamba ametuagiza kwamba tukikiri dhambi zetu kwake, Yeye ni mwaminifu na wahaki, atazisamehe dhambi zetu. (Soma I Yohana, mlango wa 1, mstari wa 9, katika ukurasa 55 katika kitabu hiki.)

_______6. Unamwamini Kristo kuwa Mwokozi wako?

_______7. Kwa kusaidiwa na Bwana utamfuata na kumwomba kila siku ili umwishie maisha yanayompendeza?

_______8. Je, utajitahidi kuwasaidia wengine kum jua Yesu kuwa Mwokozi wao?

# KRISTO ATARUDI TENA!

# UWE TAYARI



**Matayo 24:44 — "Kwa hiyo, nanyi pia, muwe tayari kwa maana Mwana wa Mtu atakuja saa msiyoifikiria."**

Read booklets online or by App
www.wmp-readonline.org

**Bure—Si Kwa Kuuza**

9-17

1006/2 Kiswahili MAT